

Sr. Agata Sobczyk SMI

**MTUMISHI WA MUNGU
SISTA MARIA DULCISSIMA
1910-1936**

Warszawa - Poland 2002
Tanzania 2010



**Mgonjwa Sista Dulcissima
akiwa na magongo ya kutembelea**

UTANGULIZI

Mada ya kazi hii ni maisha na shughuli ya Mtumishi wa Mungu Sista Maria Dulcissima (1910-1936). Kazi hii inajumuisha sura nne. Sura ya Kwanza inahusisha kipindi cha awali cha maisha ya Sista Maria Dulcissima kabla ya kupokelewa shirikani, pia historia fupi ya Shirika la Masista wa Maria Imakulata pamoja na historia fupi ya Sista Maria Dulcissima akiwa bado mtoto katika familia yake na mawasiliano yake na Masista.

Katika Sura ya Pili kitaelezwa kipindi cha malezi yake shirikani toka ukandidati, unovisi hadi kuweka nadhiri zake za kwanza. Ni kipindi cha mateso na sadaka kwa Sista Maria Dulcissima, kikiwa kimehitimishwa kwa kuyatoa maisha yake kwa nadhiri za daima.

Sura ya Tatu itaonesha mwenendo wa Sista Maria kuelekea utakatifu. Mvuto mkuu wa Sista Theresa toka Utoto Mtakatifu wa Sista Maria Dulcissima utaelewa, hasa katika maisha yake ya kiroho na uwajibikaji wake kwa kila mtu. Ugonjwa na mateso makuu vilimuunganisha Sista Dulcissima na Kristo aliyepigiliwa misumari msalabani, na aliyavumilia hayo kwa jina la upendo kwa Kristo. Yote hayo yaliendelea hadi kifo chake unyamavuni.

Sura ya Nne ni ya mwisho, nayo inaonesha kwamba ingawa amekufa, Sista Dulcissima bado angali nasi kwa kuwa roho yake bado ipo nasi. Ibada zinazofanywa na watu na wingi wa ushahidi wa watu wakimshukuru kwa msaada na fadhili mbalimbali huthibitisha kuwa kweli ni Mtakatifu. Kazi hii itahitimishwa kwa maelezo ya uanzishwaji wa mchakato wa kumtangaza Sista Dulcissima kuwa Mwenyeheri.

Muda wa kazi hii unajumuisha kipindi cha kuanzia mwaka 1910- mwaka aliozaliwa, na mwaka 1936 – mwaka wa kifo cha huyu “Mchumba wa Mungu”. Kazi hii italenga hasa machapisho na mahojiano yaliyo katika nyaraka za kumbukumbu. Kwa habari zilizochapishwa zinatoka katika nyaraka za kumbukumbu za Provinsi ya Wroclaw na Katowice pamoja na nyaraka za kumbukumbu za Nyumba Kuu ya Roma. Kumbukumbu za kihistoria za miaka katika provinsi zote zina taarifa za kutosha.

Jarida linalochapishwa na Shirika lina thamani kubwa na kwa namna ya pekee vitabu na hasa kile cha “Historia ya Shirika” kilichoandikwa na Padre Yosef Schweter kina umuhimu mkubwa. Vile vile kitabu kingine muhimu ni kile cha WANDA IZDEBSKA (Sista Anatolia) Machapisho mengine pia yanatoa taarifa za kutosha ambazo zinasaidia kuonesha dhahiri maisha na haiba ya Sista Maria Dulcissima. Hali kadhalika kazi nyingine zenye mchango mkubwa kwa kazi hii ni pamoja na mahojiano yaliyofanywa na mwandishi, barua nyingi na ushahidi uliokusanywa toka vyanzo anuai ambavyo mwandishi aliweza kuvipata.

SURA YA KWANZA

Mtumishi wa Mungu Sista Maria Dulcissima Kabla ya Kupokelewa kwa Shirika la Masista wa Maria Imakulata

1. Historia fupi ya Shirika la Masista wa Maria Imakulata

Mwanzo ya Shirika la Masista wa Maria Imakulata inaunganishwa na eneo la Silesia , hasa mji wake Mkuu – Wroclaw. Shirika liliimarishwa katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa. Ulikuwa ni muda ambao wasichana wengi walikuwa wakihama toka vijijini kwenda mijini ili kutafuta kazi. Wengi kati yao walikwenda Wroclaw. Hawakuwa na mang’amuzi yoyote kuhusu hatari za miji mikubwa na kwa hiyo mara nyingi walijihatarisha kwa mmomonyoko wa maadili; walifanya mambo ya kuzidi sana na hata kufanya uhalifu kama wizi, na hivyo kupelekwa gerezani. Wasichana wengi wa umri mdogo walikuwa katika hali hii hatarishi ya kimaadili ya wakati ule, kwamba karani ofisa wa polisi katika Wroclaw, Uhden, alimpelekea ujumbe askofu wa Wroclaw, H. Forster akiomba ili Kanisa liwatunze wasichana hao. Mamlaka ya Kiserikali ilidai kwamba ni Kanisa tu linaloweza kuingilia kati na kuweza kukomesha kuenea kwa wimbi la utovu wa maadili. Askofu Forster alilipokea ombi hilo kwa umakini mkubwa¹ akirejea maoni

¹ Mwaka 1853 Askofu Henry Forster alichaguliwa kuwa askofu wa jimbo Wroclaw. Alifariki Austria kwenye nyumba yake ya mapumziko mnamo tarehe 20 .10.1881. Alikuwa na umri miaka 82. Serikari iliruhusu masalia yake yaletwe Wroclaw na kuzikwa kwenye kaburi chini ya Kanisa Kuu la jimbo.

Sura ya Kwanza

na mapendekezo kwa Padre M. Thiel. Padre huyu alikuwa mkuwa wa dekania. Mara baada ya kupokea ombi la Askofu, Padre Thiel alitisha mkutano wa mapadre. Wakati wa majadiliano mapadre walimteua padre Yohane Schneider² kuratibu mpango hii. Padre Yohane yeye atakaye kuwa baadaye Mwanzilishi wa Shirika la Masista wa Maria Imakulata.

Padre Yohane alianza kazi yake na Makala katika “Gazeti la Kikatoliki” ambamo aliandika “Fanya hima kuokoa roho ambazo zimesimama katika ncha ya maadili yaliyopotoka, hurumieni shida nyingi za mabinti yenu³. Baada ya kuchapisha makala hii, wanawake saba waliomba kusaidia. Nao walikuwa ni: Maria Von Hoverden, Jadwiga Lehman, Emilia Hazarim, Paulina Nagel Jaschke, Franciszka Siegert, Henrietta Clemens⁴. Wanawake hawa chini ya uongozi wa Padre Yohane waliunda “Chama Cha

2. Yohane Schneider alizaliwa tarehe 11 Januari 1824 huko Mieszkowice kama mtoto wa Yohane Gregori Schneider na Katarina Fraemer. Akiwa na umri wa miaka 6 alianza elimu yake kwenye shule Katoliki huko Rudziczka. Ashukuriwe Padre A. Hoffman ambaye alimsaidia kifedha hata akaweza kuendelea na elimu ya Sekondari huko Nysa.

² Mnamo mwaka 1845 alianza masomo yake ya Kiteolojia katika Chuo Kikuu cha Wroclaw ambapo alihitimu mwaka 1848. Alipadrishwa na Askofu M. Biepenbrock mnamo tarehe 1.07 1849 na kupamgiwa Parokia Wiazow. Akiwa kama Padre Msaidizi katika Kanisa la Wiazow alianza kazi yake ya Maadili na Mafundisho ya Dini kwa Wanawake Vijana walioajiliwa katika kiwanda cha kutengeneza sigara. Baada ya miaka miwili alihamishwa kwenda Parokia ya Maria Mtakatifu Sana kwenye kisiwa cha Piasek huko Wroclaw. Mnamo mwaka 1854 alihamishiwa Parokia ya Mtakatifu Mathayo. Akiwa kama Paroko aliwatumza wale walijishughulisha na Wanawake Vijana katika Wroclaw yote.

³ M.PIETEK., *Ks. Jan Schneider I jego zgromadzenie*, 10

⁴ J. SWASTEK., *Zyjac dla innych*, 79

Sura ya Kwanza

Kulinda na Kustawisha Maadili ya Wasichana Watumishi” ambalo kwa kifupi liliitwa “Chama cha Maria”⁵

Kadiri ya Katiba cha chama, kazi ya msingi ya Chama cha Maria ilikuwa kujihusisha na mabinti waliojihatarisha kimaadili kwa kuwapatia malazi na malezi bora na pia taratibu kuwaandikisha watu walipenda kuwasaidia wasichana hao kimalazi, kifedha na kiroho. Wasichana wachache walioomba na kutaka kufanya kazi bila malipo, walijiwasilisha kwa uongozi wa kiroho wa Padre Yohane. Ndipo katika hali hii mbegu ya utawa ikatokea. Padre Yohane walipokea ombi la wasichana hawo wanne. Baada ya matayarisho ya kiroho wasichana hawa walipokea mavazi - sare ya kitawa na kuweka nadhiri zao kwa miaka mitatu⁶.



Bikira Maria Imakulata

Bikira Maria Imakulata alichaguliwa kuwa Msimamizi wa Shirika la kitawa walioanzishwa . Siku ya Kukiingwa Dhambi ya Asili Bikira Maria yaani 8 Desemba 1854

⁵ J. SWASTEK., *Zakony I zgromadzenia zakonne w zyciu diecezji Katowickiej do wybuchu II wojny swiatowej*, 305

⁶ W. IZDEBSKA., 270

Sura ya Kwanza

ikahesabika kama ndio mwanzo wa Shirika, na kwa sasa inasherehekewa kama ndio siku ya Somo mtakatifu wa shirika⁷ Mwanzilishi alisititiza masista wafuwata mfano wa Bikira Maria na aliwekwa picha ya Bikira Maria wa Czestochowa katika kikanisa kidogo cha nyumba yao mwaka 1866. Baadaye aliweka picha ya Bikira Maria Imakulata Msimamizi wa Shirika.

Mnamo mwaka 1864, Masista chini ya uongozi wa Padre Yohane, walimchagua Mama Mkuu yawo, naye alikuwa ni Sista Matylda Scholz. Baada ya uchaguzi Padre Mwanzishi alituma katiba ya Shirika kwa kiti cha Kipapa kwa kuthbitisha. Tangazo la Sifa, hati ambayo Shirika la Masista wa Maria Imakulata lilipata uthibitisho wake wa kwanza toka Roma, ambalo lilitolewa mwaka 1897⁸.

Mnamo 1869 askofu wa Wroclaw aliitambua jumuiya ya Masista wa Maria Imakulata kama moja ya Mashirika yaliyo chini ya jimbo. Kazi nzito za Padre Yohane zilisababisha kifo chake hapo 7 Desemba 1876⁹.

Wakati Mwanzishi anafariki, kulikuwa na masista tisa tu kwenye shirika. Kwa hakika kifo chake kilileta majonzi makubwa sana miongoni mwa mabinti maskini ambao kwao alikuwa kama baba, na miongoni mwa masista pia ambao walimpoteza kiongozi na baba yao wa kiroho. Askofu Foster kutokana na kifo cha Padre Schneider, alisema: “Alikuwa pambo miongoni mwa wachungaji, kwa ibada yake, nguvu ya utayari wake na maisha yake ya ndani”¹⁰.

⁷ B. LOZINSKI., *Leksykon Zakonow Polsce*, 251

⁸ W. IZDEBSKA., Tz

⁹ Słownik biograficzny katolickiego duchowienstwa slaskiego XIX i XX wieku, pod red. M. Petera, Katowice 1996, s. 370

¹⁰ J. COP, *80 lat obecności Siostr Maryi Niepokalanej w Brzeziu na Odra*, 7

Sura ya Kwanza

Mnamo 1969 masalia ya Padre Schneider yaliamishwa toka makaburi ya Osobowice na kupelekwa kwenye Kanisa la Bikira Maria kwenye kisiwa cha Piasek huko Wroclaw¹¹.



Padre Yohane Schneider

Wakati wa miaka ishirini ya mwanzo Shirika lilidorora sana lakini baadaye kwa bahati njama maendeleo yalianza. Nafasi ya Padre Mwanzishi walichukuwa Wasimamizi kutaka jimbo. Wao walijaribu kwa uwezo wao wote kuiendeleza kazi hii¹². Maendeleo ya haraka ya Shirika yalitokea hasa katika eneo la jimbo la Wroclaw. Mnamo mwaka 1898 Shirika lilikwenda nje ya jimbo likianzisha shughuli yake Hospitali ya Magonjwa ya akili huko Branice iliyoanzishwa na Padre J.M. Nathan¹³

Mnamo mwaka 1929 kituo cha kwanza katika eneo la jimbo la Katowice kiliimarishwa. Nyumba hiyo ilibarikiwa

¹¹ ADMSMNW, *Okolnik Matki Generalnej, Builetyn Zgromadzenia Siostr Maryi Niepokalanej*, Wroclaw 1969, nr 1, s.6

¹² S. E. BANIK., *KITABU W Sluzbie Niepokalanej*, 26

¹³ ADMSMNW, *Zyjac dla innych*, 99

Sura ya Kwanza

na Kardinali A. Bertram, na kuwekwa kuwa makao ya Shirika ya Provinsi ya Poland¹⁴.

Umuhimu mkuu wa kuwaelimisha wasichana ulikuwa na heshima kwa Bikira Maria. Miongoni mwa mambo mengine, njia za kuwaelimisha zilijumuisha kushiriki katika ibada kanisani, masomo ya katekesi na kuhusika katika maadhimisho na maonyesho mbalimbali ya kidini¹⁵.

Kazi ya Padre Yohane ilianza kuwa na uhai mkubwa. Masista wa shirika waliendeleza shughuli yao kati ya wasichana kadiri ya mpango wa muhtasari wa Padre Schneider¹⁶.

Masista walishirikiana na Chama Cha Kulinda na Kustawisha Maadili ya Wasichana Watumishi (Chama cha Maria) na Mashirika mengine ya Kikatoliki ambayo yalikuwa yakiwatunza wasichana katika majiji, ambamo matatizo yalikuwa yakiongezeka wakati ule. Shughuli hiyo ilifanika katika vituo vya reli ambako wasichana waliwasili mjini na treni. Wao walipata ushauri na huduma ya kwanza. Wasichana ambao hawakuwa na sehemu za kuishi wakielekea kwenye nyumba ya Chama cha Maria na kupata mahitaji muhimu.¹⁷

Wakati Vita vya Pili vya Dunia vilipoanza, shughuli za Masista wa Maria zilikatizwa, hata kuzuiliwa. Uchungu na maumivu waliyoyapata Masista wakati wa vita yalipelekea hata vifo kwa baadhi ya wanashirika. Nyumba yao Mama

¹⁴ J. SWASTEK., *Zyjac dla innych*, 99

¹⁵ Mwanzishi alitimiza malengo ya elimu kwa kutoa zawadi kama mbinu. Kwa namna hii aliendeleza ushindani kati ya wasichana, wakiibua hali ya kujiamini na kutumaini na hivyo kuimarisha mahusiano ya kielimu kati yao. Zawadi hizo zilitolewa wakati wa maadhimisho muhimu ya Chama cha Maria mbele ya wanachama wote.

¹⁶ O. J. SCHWETER., *Historia Zgromadzenia Sióstr Marianek*, 51

¹⁷ APSMKNK, *Kronika Prowincji Polskiej Zgromadzenia Sióstr Maryi Niepokalanej*, 17

Sura ya Kwanza

huko Wroclaw ilipigwa bomu na sehemu nyingine ilichomwa moto.

Baada ya vita, kwa ujumla ilikuwa vigumu sana kuratibu maisha ya kawaida ya utawa huko Poland, na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Masista wa Maria Imakulata. Kilele cha hayo yote kilikuwa ni mwaka 1954. Mwaka ule, shughuli za Shirika zilizuiwa kwa kuwatawanya masista na kunyang'anya nyumba zao za kitawa kinyume cha sheria. Waliichukua kambi ya kazi huko Otorowo karibu na Poznan ambako waliikalia kwa muda wa miaka miwili.

Kwa kutengwa na watu, kukatazwa kutumia redio na magazeti, na kwa kuwa chini ya ulinzi wa maafisa wa usalama wa Kikomunisti. Masista walifanya kazi kwenye chumba cha kushona chini ya amri ya wasimamizi. Mwanzoni mwa mwaka 1957 waliruhusiwa kuondoka kambini na kurudia nyumba zao za kitawa lakini sio zote ukizingatia kuwa nyumba zao nyingi zilitaifishwa. Mwaka 1954 wakati Masista walipopelekwa Otorowo, wanovisi na wakandidati walirudishwa nyumbani kwa wazazi wao. Lakini baada ya muda walirudi Shirikani sehemu walizopangiwa.

Mwaka 1963 mara ya kwanza baada ya vita Mkutano Mkuu wa Shirika ulifanyika Roma. Mkutano ulipitisha maamuzi kuhamisha Nyumba Mkuu ya Shirika huko Roma, jambo lililofanyika mnamo mwaka 1970¹⁸.

Tangu mwaka 1972 Masista wamekuwa wakifanya kazi Afrika - Tanzania na kutimiza wosia wa Mwanzilishi: „Fanya hima kuokoa roho ambazo zimesimama katika ncha ya maadili yaliyopotoka, hurumieni shida za mabinti, Kituo chao cha kwanza cha kazi kilikuwa ni Kilimarondo. Mwaka 1976 nyumba ya pili ilifunguliwa Nanjota Kusini mwa Tanzania karibu na mpaka wa Msumbiji. Toka wanaanza

¹⁸ J. SWASTEK., *Zyjac dla innych*, 102-104

Sura ya Kwanza

Masista waliweka nguvu katika dhamira ya shirika kwa kufanya kazi pamoja na wasichana, wanawake na watoto. Wanaongoza shule za awali za watoto wadogo, wanatoa mafundisho ya dini, wanafundisha kushona, kazi za mikono, mapishi, kuwatunza wagonjwa hospitalini na huduma ya afya ya mama na mtoto¹⁹. Baada ya muda nyumba ya Kilimarondo imefungwa. Sasa Masista wanafanya kazi Chikukwe ,Nanjota, Dar es Salaam ,Morogoro na Mwanga.

Katika ulimwengu wa leo kuna mijeledi isiyo na idadi: pombe na kubobea katika madawa ya kulevya, picha chafu za ngono, umalaya. Wahanga wa mambo haya mara nyingi ni vijana. Masista wa Maria Imakulata wamejiingiza katika shughuli za mafungo ya kiroho, “siku za tafakari” kwa vijana. Kama washauri wa kujitolea wanafanya kazi katika nyumba “Malaika Walinzi” nyumba hii ni ya kutwa huko Katowice. Ni kazi inayojihusisha na vijana waliobobea katika madawa ya kulevya, watoto waliojiingiza katika umalaya ambapo baadhi yao hawana makwao, hawana yeyote, hawana pa kwenda. Wapo ambao walitoroka nyumbani, watoto ambao wamekulia “mitaani”²⁰.

Masista wa Maria wanafuata sauti ya Mungu, wanatambua wito wao na kutimiza majukumu yao ambayo wamekabidhiwa katika utume na shughuli za Shirika. Wanaendeleza shughuli hii kwa huduma yao watoto katika chekechea, nyumba za watoto yatima watoto wenye wanaohitaji uwagalizi wa pekee. Wanaipeleka huduma yao kwenye nyumba za wazee, makazi ya watu, na hospitali. Vilevile wanawasaidia kazi za Mapadre. Wanafundisha dini shuleni na kuongoza makundi ya vijana hasa wasichana.

¹⁹ Biuletyn, Rzym 1984, nr 15, s. 8-10

²⁰ ZPA, S. Anna Balchan

Sura ya Kwanza

2. Nyumba ya Familia – Utotoni

Helena Joanna Hoffmann alizaliwa tarehe 07th Februari 1910 huko Eintrachthutte (Zgoda), Wilaya ya Swietochlowice katika familia ya wafanyakazi. Baba yake, Yosef Hoffman, alikuwa ni Mjerumani, ambaye alizaliwa huko Gasiorowice wilayani Strzelce Opolskie, lakini aliweza kuzungumza Kipolandi. Mama yake Albina Nee Jarzebek, alikuwa ni mwenyeji wa kuzaliwa wa Zgoda – alikuwa Mpolandi²¹.

Nyumba ya Familia




Helena alibatizwa na paroko msaidizi Padre Francisko Sitko tarehe 13 Februari 1910 katika kanisa la Mtakatifu Yosefu huko Zgoda Swietochlowice. Wasimamizi wake

²¹ Baba yake Helena alizaliwa 08th Septemba 1886 huko Gasiorowice. Alikwenda Silesia ya Juu pamoja na kaka zake. Alikaa katika mkoa wa Eintrachthutte karibu na kiwanda cha chuma cha “Zgoda”. Akiwa pale alikutana na Albina Jarzebek ambaye alizaliwa 31st Desemba 1889. Walifunga ndoa katika kanisa la Watakatifu Petro na Paulo huko Swietochlowice mwaka 1909. Walifanya makazi yao katika nyumba ya kifamilia iliyoitwa “familiok”

Sura ya Kwanza

walikuwa Marta Plutzik na Feliks Hofman toka Swietochlowice²².



**Kanisa la Mtakatifu
Yosefu ambapo Sista
Dulcissima alibatizwa**



Wazazi wa Sista Dulcissima

²² Baptism book, 1910r., nr 110.

Sura ya Kwanza

DIECEZJA
Parafia **Rzymsko-Katolicka Parafia** **ŚWIADECTWO CHRZTU**
..... **św. Pawła** (Testimonium baptismi)
Adres **41-709 Ruda Śl.-Nowy Bytom** **Dla celów kościelnych**
..... **pl. Wolności Nr 5-tel.487-553**

1. Rok i numer księgi ochrzczonych **1910/110**
(Annus et numerus libri baptizatorum)
2. Imię i nazwisko **Helene, Johanna Hoffmann**
(Nomen, cognomen)
3. Imię ojca **Josef**
(Nomen patris)
4. Imię matki **Albine geb. Jarzombek**
(Nomen matris)
5. Miejsce i dzień urodzenia **Eintrachthütte 7.02.1910**
(Locus et dies nativitatis)
6. Miejsce i data chrztu **Eintrachthütte 13.02.1910**
(Locus et dies baptismi)
7. Uwagi w księdze ochrzczonych (kan. 535 § 2, 1685) **Conf. 5.5.1927 Zgoda "Teresia"**



Zgodność z miejscową księgą ochrzczonych potwierdza
(Concordat cum libro baptizatorum)

N. Bytom dnia **17. 12.** 19**97**
(die)

Fr. J. Górczyński
(Proboszcz — Parochus)

Cheti cha Ubatizo

Helena alikuwa ni kifungua mimba. Baada ya miaka miwili, Mungu alimjalia Hoffman mtoto wa kiume ambaye aliitwa Reinhold. Ndugu hawa waliishi pamoja kwa amani. Reinhold alimheshimu sana dada yake na alifuata mfano wake, akiiiga hekima yake. Baba yao alikuwa ni mtu wa moyo mkuu, lakini mkali, na wakati mwingine alikuwa mkali sana, hata kwa mkewe na kwa baba zake wadogo wane ambao alikuwa akiwatunza. Alikuwa vile vile mkali sana hata kwa watoto zake. Alikuwa makini kwao ili wawe na mwenendo mwema na tabia za staha. Wakati wa matembezi watoto walitangulizwa mbele ya wazazi wao, wakiwa wameshikana mikono. Na wakiwa wanatembea mtaani hawakuruhusiwa kuongea wala kutazama nyuma.

Sura ya Kwanza

(Kuangalia huko na huko)Wakiwa mezani, watoto hawakuruhusiwa kuanza kula kabla ya baba yao kuketi na kuanza kula. Hivyo, watoto iliwapasa wawe watii kwa baba, vinginevyo waliadhibiwa vikali. Sista Dulcissima baadaye aliandika: Utashi wangu ulishavunjika tangu utoto wangu²³. Toka amri za wazazi alitambua sauti ya Mungu na alimfundisha mdogo wake kutii matakwa ya wazazi wao.

Akiwa na umri wa miaka sita, Aprili 1916, Helena alijiunga na shule ya msingi kiktoliki. Alikuwa na uwezo wa kuzungumza Kipolandi na Kijerumani. Alikuwa ni mwanafunzi mwenye bidii na alama nzuri darasani. Biblia Takatifu na Katekisimu yalikuwa ni masomo aliyoyapenda sana²⁴. Katika masomo yake ya dini alimakinikia juu ya Mungu Mwokozi, ambaye alimpenda. Kwa hiyo muda wake mwingi wa ziada alitumia kanisani. Akiwa pale, alielekeza macho yake moja kwa moja kwenye tabernakulo na kusali kwa muda mrefu. Vilevile alikuwa akipiga magoti mbele ya altare ya Mama wa Mungu.

Katika kipindi cha shule baba yake alimwita Helena “katukutu kadogo”. Mama yake alimwita “Mwanasesere mtoto”. Ilipotokea kuwa Helena alitoroka shuleni, bila ya kuwa na sababu yoyote ya ugonjwa, ingawa bado alijihisi mwenyewe kuwa amekimbilia kufanya kitu kizuri. Tabia kama hiyo ya kutoroka shuleni kwa mfano, mara nyingi ilifuatiwa na adhabu. Hakukukuwa na siku hata moja – Helena anasema – ambayo sikufanya utukutu²⁵.

Mnamo mwaka 1919 baba yake Helena alifariki. Katika hali ya uchungu wa shukrani Sista Helena alikumbuka kazi za awali za mama yake mjane, wajibu zake

²³ O.J. SCHWETER., *Oblubienica Krzyza*, 10

²⁴ J. COP., - S. M. A. PLACZEK (SMI), *80 lat obecnosci Siostr Maryi Niepokalanej w Brzeziu nad Odra*, 33

²⁵ A. KIELBASA SDS, *Droga do swietosci Siostry Maryi Dulcissimy Hoffman 1910-1936*, 133-114

Sura ya Kwanza

na mateso. Aliandika: “Baada ya kifo cha baba yangu, wadogo zake baba walitawanyika. Mama yangu ilimbidi afikiri namna ya kutusaidia. Wakati huo mdogo wangu alikuwa na umri wa miaka 7 na mimi likuwa na umri wa miaka 9 tu. Mama yangu alikuwa na umri wa miaka 29 tu wakati alipokuwa mjane. Akiachia huruma ya Mungu, akawa mama na baba pamoja kwetu sisi. Sikuwa na mashaka wakati wowote ni kwa nini haya yalitokea. Sasa nilikumbuka siku za utoto wangu wakati ambapo mara nyingi nilisema kwamba nitamsaidia mama yangu kazi za nyumbani. Ili kumfurahisha, nilijaribu kufanya yote ambayo alifanya na nilijifunza toka kwake kuchoma mkate, kufua, kusuuza au kutia wanga za ndani zilizotundikwa kwenye kigoda na mambo mengine”²⁶.

Kifo cha ghafla cha baba yake kilikuwa ni pigo kubwa kwa Helena. Yeye mwenyewe kuhusu hili alisema: Ilikuwa ni furaha halisi kuishi pamoja katika familia. Yesu alikuwa na mipangilio mingine kwa mama yetu na sisi watoto; amemchukua baba yetu mpendwa. Baba alikuwa mgonjwa kwa siku chache tu. Alipoindea nchi ya milele ya Baba pale tarehe 08 Januari 1919 alikuwa na miaka 32 tu. Akiwa amelala kitandani, alichukua maji ya baraka, akajipiga mwenyewe ishara ya msalaba mara tatu na kusema: Sitainuka tena. Hofu kuu ilimshika mama yangu, akasema: Lakini hutakufa! Wakati baba alipomhitaji padre na kupenda aje kabla ya Misa kuanza, mama yangu alimwitia haraka. Wakati padre akiwa njiani, baba alipoteza fahamu. Kulikuwa na muda ambapo alisema kitu fulani, kujibu maswali kwa kuitikia kwa kichwa kidogo. Vile vile alidai kwamba kaka yake Franciszek awe kama baba kwetu. Baba mdogo Franciszek akiwa jeshini wakati ule, mama alimpigia simu. Wakati alipofika, baba yangu alifungua

²⁶ J. SWASTEK, *Zyjac dla innych*, 144

Sura ya Kwanza

macho yake na kusema: Chukua kila kitu na usimwache mke wangu na watoto. Baba mdogo Franciszek aliingiwa na hofu. Baba alifariki saa nane usiku. Mwanzoni kifo chake kilifikiriwa kuwa ni kifo cha uongo hivyo siku ya mazishi iliahirishwa. Hata hivyo, baba yangu alikuwa kwenye umilele tayari²⁷.

Baada ya muda wa maombolezo kupita, baba mdogo wa zamani akawa Baba mlezi wa Helena na Reinhold. Sio kwamba tu walikubali ndoa ya pili ya mama yao, bali pia kwa furaha mara walimkaribisha katika familia yao kaka mpya aliyelitwa Henryk,²⁸.

Akikumbuka mahangaiko ya mama yake, Sista Dulcissima aliandika: Mwishoni mwa Januari 1919 homa kali ya kichwa ilitokea. Akiambatana na Baba mdogo Franciszek, waliwatembelea wazazi kule Gasiarowice. Baba mdogo Franciszek alipatwa na homa kali ya kichwa wakiwa kule na alirudi akiwa mgonjwa. Nyumba yetu yote ilizingirwa na polisi na kwa sababu kila mpangaji aliugua na wote walipelekwa kwenye vibanda vya muda pamoja nasi huko Nowy Bytom.

Tukajikuta tuko hospitali. Tulikuwa tumetengwa na kufungiwa katika chumba chenye madirisha yenye nondo. Kwa siku za mwanzo tulipewa huduma nzuri lakini mara tulithibitishiwa kuwa hatukuwa na uwezo wa kulipia matibabu yetu. Kwa kuwa mama yetu alikuwa mjane, tuliondolewa marupurupu yote tuliyokuwa tunapewa. Lakini hata hivyo Mungu alikuwa akitutunza. Ilimbidi mama yangu afanye kazi kwa bidii hospitalini; ilimbidi awe anapakua makaa ya mawe au kutoa maji kisima cha chini cha chumba cha kuhifadhia maiti hospitalini. Moyo wake ulionekana kana kwamba umechomwa kwa mkuki. Baada ya miezi

²⁷ O. J. SCHWETER, *Oblubienica Krzyza*, 12-13

²⁸ Biuletyn, Rzym 1996, nr 23, s. 38

Sura ya Kwanza

mitano ya uangalizi, tuliruhusiwa kuondoka. Wakati tuliporudi kwenye nyumba yetu hali ikawa si nzuri kabisa: madirisha yalijifunga, nguo za ndani na manyoya ya somateria vilitawanyika kila mahali, ng'ombe na zizi viliharibika na matumaini aliyokuwanayo mama yetu, yalipotea. Ninakumbuka jinsi alivyoutazama msalaba na kujiambia mwenyewe: “nitayaanza upya haya yote, kwa unyofu na busara, ili kwamba nibaki kuwa mama yule yule”. Hakulalamika wala kunung'unika; hakutafuta watu wamsaidie; alitaka kutimiza mapenzi ya Mungu tu²⁹.



Helena akiwa mdogo katika umri wa shule

Toka nyumbani Helena alijifunza imani imara, misingi ya maadili mema, upendo na uangalifu katika kazi, na zaidi ya yote, hisia nzito kwa kila hali ya mateso. Akiwa mtoto, mara nyingi alilia bila ya kuwa na sababu yoyote. Baadaye akiwa shirikani aliandika: “Sasa nafikiri ni Mungu tu ambaye nilikuwa nikimtafuta na bado sijamfahamu sasa; nao ulikuwa ni ujinga huu ambao ulinifanya niwe nikilia. Pamoja na kulia huku kote, bado sikufahamu, na ndio

Sura ya Kwanza

maana niliadhibiwa mara kwa mara”³⁰. Wazazi nao hawakuelewa tajriba ya kidini ya mtoto wao. Kwani ilikuwa ni Mungu aliyekuwa akinena katika kilio cha mtoto huyu mdogo. Mtoto Helena alisali sana. Kama msichana mdogo, alipenda kuirushia maua Ekaristi Takatifu katika Sherehe ya Mwili na Damu ya Yesu.

Akiwa na umri wa miaka 10, mwishoni mwa mwaka 1910, akitayarishwa na Paroko huko Zgoda, Helena alipokea Komunyo ya Kwanza. Padre aliwaeleza watoto kuhusu Maungamo; kwamba wanapaswa kujenga kikanisa cha kiroho kwa ajili ya Mungu Mwokozi kwa kufanya mazoezi wao wenyewe kwa baadhi ya fadhila. Helena alilielewa jambo hilo na alitoa ushuhuda kwa maandishi wakati wa Komunyo yake ya Kwanza. Tajriba (uzoefu) ile ilikuwa msingi kwa maisha yake yote³¹.

“Mwishowe, siku ya Komunyo ya kwanza iliwadia – yaani tarehe 5 Mei 1921. Kwa sababu ya kazi zake ngumu, mama yake alichoka sana na kuwa mgonjwa. Hivyo alimpatia pesa mtoto Helena na kumwambia: “Nenda kajinunulie kitambaa cheupe kwa ajili ya gauni la Komunyo yako ya Kwanza”. Baadaye Sista Dulcissima aliandika - “Nilikwenda dukani na kuomba kitambaa cheupe. Kwa kuwa nilikuwa msichana mdogo, nilihisi kama kwamba nimepotea kati ya watu. Mwuzaji wa duka aliniangalia kwa mshangao na kuniuliza: “Mama yako yuko wapi?” Nilidhaniwa kuwa nimeiba fedha. Sikukubali kuadhiliwa namna ile, nililia kwa sauti na kusema: “Ikiwa kesho (Jumapili) duka halitafungwa, nitakuja na mama yangu”. “Kisha nikapata kila kitu, hata ugwe matambara (riboni) ambao sikutakiwa kuulipia”³².

³⁰ Ibid., 10

³¹ J. SWASTEK., *Zyjac dla innych*, 114

³² O. J. SHWETER., *Oblubienica Krzyza*, 15

Sura ya Kwanza

Helena alisukumwa sana na maneno ya Padre Edward Adamaczyk kuhusu „kujenga kikanisa” kiasi kwamba alikumbuka yote katika maisha yake. Hata wengine waliweza kuona katika historia ya maisha yake “Kikanisa Changu”. Kabla ya matukio hayo makuu, Helena aliota kuhusu kuwa mtawa. Mara nyingi aliirejea ndoto hiyo³³.

Kwa mtoto Helena, siku ya Komunyo ya Kwanza ilikuwa ni siku ya furaha kuu. Ilikuwa ni siku kubwa kiasi kwamba hakufikiri kitu kingine chochote; wazo pekee lilikuwa ni kwamba “Yesu atakuja kwangu mara, na nitakuwa na tabernakulo katika kikanisa changu!” Mamaye akiona furaha yake alisema: “Utakuwa mgonjwa wa upendo baadaye”³⁴.

Komunyo ya Kwanza



³³ O. J. SHWETER., *Oblubienica Krzyza*, 6

³⁴ A. KELBASA, *Droga do swietosci Siostry Maryi Dulcissimy (1910-1936)*, 115

Sura ya Kwanza

Baada ya maadhimisho kanisani, mamaye alimjia na kumwuliza: “Kwa nini hutoki nje? Sisi sote tunakusubiri”. Lakini Helena hakujua aseme nini. Alikuwa na furaha mno. Siku iliyofuata kwa uangalifu sana alimwuliza mama yake: “Umekuwa ukifanya nini na hostia kila baaya ya kukomunika?” Mama yake alimjibu: “Nilijua kwamba umpumbavu mwanangu, lakini huo ni upumbavu wa kuzidi. Hujui kwamba Yesu katika Hostia Takatifu anakuwa ameliwa?” Unyenyekevu huo haukumfanya mtoto Helena kuwa na huzuni, kinyume chake alijisikia furaha kwamba mama amemwambia kitu hicho waziwazi. Mungu alimzawadia Helena jambo hilo kwa namna wazi.³⁵ Siku moja akiwa anafanya kazi shambani pamoja na wazazi wake, aliiona nishani kubwa yenye picha ya mtawa kijana akiwa na mauaridi kifua ni mwake. Mara Helena akatambua kuwa yule mtawa alikuwa ni sawa na yule aliyemwona katika ndoto kabla ya Komunyo yake ya Kwanza. Ingawa jambo hili lilikuwa ndoto, alipata hisia ya moyo na furaha ya ndani. “Ilikuwa ni msaada kwangu katika kujenga kikanisa changu kwa mazoezi na sala, ambao nimeagizwa kwa ufunuo ule. Nilikuwa nikisali sana na kwa moyo ili kwamba asiwepo yeyote ambaye angeweza kufahamu nini kilitokea. Nilikua nikijenga kikanisa changu kwa siri kwa ajili ya Mwokozi, ili kwamba kijulikane na yeye tu”³⁶.

Kwa kiasi hicho, mtoto Helena hakumweleza yeyote kuhusua ufunuo na nishani hii kubwa. Hii haiwezi kuwa njozi zozote, akiwa kama msichana mdogo, hajawahi kusikia chochote kuhusu Sista Theresa wala kuona picha yake. Ni kwa muda fulani tu alijifunza habari ya mtawa anayefanya miujiza na kuona picha yake katika majarida ya

³⁵ O. J. SCHWETER., *Oblubienica Kryza*, 16

³⁶ O. J. SCHWETER., *Oblubienica Kryza*, 17

Sura ya Kwanza

kidini. Baadaye, katika moja ya ndoto zake, Theresa wa Mtoto Yesu alimtokea Helena³⁷.



Helena shuleni

Watoto shuleni walimpenda Helena, alikuwa na akili sana na aling'ara kama jua. Daima alishika nafasi ya kwanza katika masomo ya dini. Mara nyingi alijihusisha katika maonesho mbalimbali au kughani mashairi katika maadhimisho ya sherehe mbalimbali, hata kama kinyume cha mapenzi ya wazazi wake. Hii iliwapatisha wivu wenzi wake na baadhi ya watu wazima, na matokeo yake mara nyingi alipata tabu na alilia wakati hali hiyo ya huzuni ilipompata³⁸.

Wakati mwingine alikuwa akisaidia parokiani. Tangu akiwa mtoto alijisikia kuwa na wajibu wa kuwasaidia mapadre. Baadaye aliweza kusema: Nilikuwa nimekaa parokiani nikalala chumba cha darini. Huko nililala chini, bila kitanda, ilijiviringishia kitu fulani nakuweka chini ya kichwa changu. Paroko wangu hajajuwa kama ninafanya

³⁷ O.J. SCHWETER , *Oblubienica krzyza*, 16

³⁸ J. SWASTEK, *Zyjac dla innych*, 116

Sura ya Kwanza

hivyo. Nilikula kwa shida, kidogo sana kwa hivyo nimekonda sana na mama yangu hakuniruhusu tena kukaa pale. Alimwambia Paroko ‘Yeye angali mdogo mno kufanya kazi sana’ Paroko hakufurahia kuondoka kwangu, na alihuzunika sana aliniona ninaondoka³⁹.

Wakati fulani kulikuwa na padre aliyetembelea Zgoda. Mara nyingi aligonga mimbari wakati wa mahubiri yake, kitu ambacho mtoto Helena alikichukulia kama si sahihi. Kwa hiyo aliweka misumari kidogo chini ya kitambaa cha meza akienezea mimbari yote ili kumfundisha kwamba asiwe anafanya “mapigo” yale tena. Mhubiri alimweleza paroko kuhusu suala hilo. Paroko alijua mara, kwa hisia, “mwovu” huyo alikuwa nani. Helena, akiwa amelazimishwa na paroko kukubali alisema: “Ndiyo, nakubali, kwa sababu nadhani kwamba si kitu sahihi kugonga mahali ambapo Mwokozi anaishi. Usifanye hivyo na siafiki kufanya hivi katika kanisa letu vilevile”⁴⁰.

Tarehe 1 Desemba 1923, Helena Hoffmann alihitimisha masomo yake kwenye shule ya serikali huko Zgoda. Katika taarifa yake ya shule alipata (Vema Sana) katika maadili na na masomo mengine yote, kujumuisha Kipolandi na Kijerumani, alipata B (Vema)⁴¹.

Tarehe 5 Mei 1927 Helena alipokea Sakramenti ya Kipa-Imara, iliyotolewa na Askofu Arkadiusz Lisiecki, huku akichukua jina la Mtakatifu Theresa wa Mtoto Yesu. Kwa upande mwingine alitambua kuwa tangu muda ule alipaswa kuwa chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu; kwa upande mwingine chaguo la Mtakatifu Theresa lilikuwa ni mwendelezo wa ibada ambayo tayari alishaianzisha.

³⁹ O. J. SCHWETER, *Oblubienica krzyza*, 19

⁴⁰ Ibid., 19

⁴¹ Ibid., 117

Sura ya Kwanza



Helena kwenye Chama cha Maria

Baada ya Kipa-Imara Helena alijiunga na Chama cha Maria ambapo lilirejea wazo lililounganishwa na Kukingiwa Dhambi ya Asili. Wanachama wa Shirika walisali sala zao ambazo ziliwasaidia kunsifu Kukingiwa Dhambi ya Asili na sala hiyo iliwakinga dhidi ya dhambi. Mara nyingi walisali sala hizo hivi: “Ee Maria, uliyepata mimba bila ya kuwa na dhambi, utuombee sisi tunaoutafuta msaada wako” au “Ee Mama yangu! Ee Mama yangu! Kumbuka kuwa mimi ni wako! Uniokoe, unilinde, kama kitu chako na mali yako”⁴².

Wakati ule, wito wake wa mtawa uliendelea kukua na kukua. Mnamo Jumapili ya Utatu Mtakatifu ya mwaka 1925, alijikabidhi mwenyewe kwa Utatu Mtakatifu na kujumuisha ombi la moyo wake kwa maisha ya kitawa katika tendo hili⁴³.

Katika ndoto, Theresa wa Mtoto Yesu, ambaye alitangazwa mtakatifu wakati ule, alimwonyesha Helena kipande cha shamba ambalo alipaswa kushirikiana naye

⁴² Parish archives 1890-1927

⁴³ O. J. SCHWETER., *Oblubienica Krzyza*, 22

Sura ya Kwanza

kulilima. Helena alifanya karibu kazi zote: kufunika udongo, kutupa mbali mawe, kuleta maji, na yeye Theresa ilikuwa ni kumwagilia na kupalilia tu. Theresa alilimbika haki yake ya kuigawa bustani. Alitoa ushauri, maelekezo, kazi za kufanya na vile vile mazoezi katika fadhila na kusali ili Helena aweze kuyatimiza hayo mpaka watakapokutana tena⁴⁴.

3. Mawasiliano yake ya mwanzo na Masista

Masista wa Maria Imakulata waliletwa Zgoda na Paroko Edward Adamczyk pale tarehe 31 Januari 1920. Mwanzoni masista walifanya kazi huko Swietochlowice ambako baadaye nafasi yao ilichukuliwa na Masista wa Mtakatifu Boromeo; na Masista wa Maria walijishughulisha na kwenye kazi ya uchovyaji wa chuma Zgoda. Mara nyingi Helena aliwasaidia, hasa kwa kupamba kanisa, kufua nguo za kanisa, kupamba altare kwa maua, kuwaomba maua wanaparokia, n.k. Hakukuwa na jambo lolote gumu kwake kulifanya. Muhimu ya yote ni kumfanya Yesu afurahi⁴⁵.

Masista waliishi katika nyumba ambapo hospitali maalum ya wagonjwa wa kiwanda cha chuma „Zgoda” wasiolazwa hospitalini ilikuwapo. Sehemu hiyo iliitwa Makazi ya Mtakatifu Maria. Walikuwa wakifanya kazi za uuguzi kwa wagonjwa, hasa katika Hospitali ya Zgoda. Vile vile walikuwa wakiwatembelea magonjwa chumbani mwao na kuendesha kazi za mikono shuleni na katika jiko la serikali. Vile vile walijishughulisha na mambo mbalimbali ya parokia huko Zgoda na kuendesha chekechea. Helena alikuwa akiwatazama masista na kazi zao. Kadiri ya

⁴⁴ Ibid., 44

⁴⁵ J. GORECKI, *Parafia sw. Pawła w Nowym Bytomiu*, 10

Sura ya Kwanza

masista, alikuwa msaada na alikuwa na moyo wa uangalifu kwa maskini akiwa mtoto mchangamfu sana⁴⁶.

Masista walimpenda sana Helena. Wakati wa Noel mwaka 1920, Helena, ambaye alikuwa akifanya kazi katika chekechea, alitaka kumfurahisha sista Tobia. Akiwa na msichana mwingine waliwatembelea wazazi wa watoto wa chekechea na kukusanya fedha ambazo alizitumia kwa kumnunulia kandambili sista Tobia. Aliwapatia kama kitu cha kisasa. Alitarizi kanzu ya kasisi akisali na kutolea kila mshono kwa Yesu na Maria na mara nyingi aliimba muda wote⁴⁷. Baada ya kuhitimu shule ya serikali, Helena aliwaeleza wazazi wake kuwa atajiunga na Shirika.

Safari ya kuelekea nyumba ya utawa ilikuwa ngumu kwa Helena, kwa mama yake, na vile vile kwa watu waliompinga. Kila kitu kilionekana kuwa ni njama dhidi yake lakini hawakuweza kumshinda. Kadiri ya maadili ya Helena, Paroko Padre Jan Pacha kutoka Zgoda alitoa ushuhuda huu: “Nilimfahamu Helena Hoffmann kama msichana mwema tokana na maadili yake angavu na kwa unyofu naweza kumthibitisha kwa Waheshimiwa sana Masista wa Maria Immakulata. Alipata Kipa-Imara hapa, tarehe 07 Desemba 1927”⁴⁸.

Mganga mkuu wa hospitali ya kazi za kiwanda cha chuma cha pua huko Rozdzien alimkadiria bayana matokeo ya uchunguzi wa uwezo wa akili. Katika msingi huu, kadiri ya ombi lake kuu, Helena alipokelewa kwenye Shirika la Masista wa Maria Immakulata kama mkandidati tarehe 7 Desemba 1927.

⁴⁶ O. J. SCHWETER., *Oblubienica krzyza*, 18-19

⁴⁷ Ibid.,

⁴⁸ Cit. Za J. SCHWETER., *Oblubienica krzyza*, s.22

SURA YA PILI

Malezi ya Kitawa

1. Ukandidati na Unovisi

Ilikuwa ni jitihada ngumu sana kwa Helena kupata kibali cha wazazi kuingia shirikani, jitihada ambayo ilimtunukia shukrani kwa uvumilivu wake katika sala tulivu kama mfano bora wa fadhila. Paroko wa pale alipenda kumwona kama mkandidati katika Shirika la masista wa Mt. Karoli Baromeo huko Bytom. Masista hawa wailikuwa ikijishughulisha na elimu na kuwafundishia wasichana maskini. Hata hivyo, kulikuwa na nguvu isiyozuilika iliyomsukuma Helena kuelekea Masista wa Maria Imakulata, ambayo Mtakatifu Theresa alimpatia ili awaze kuelewa. Kadiri ya mapenzi ya Mtakatifu huyu wa Lissieux, ilimpasa Helena kutoa sadaka kwa Kanisa, Mapadre na Masista wa Maria Imakulata. Katika maandishi yake yaliyojulikana kwa jina la “Kikanisa Changu”, alirejea kipindi cha nyuma cha maisha yake: “Nilikuwa na magumu dhidi ya wazazi wangu ambao hawakuniruhusu kupokea Komunyo mara nyingi. Nikibubujikwa moyoni, nilimpokea Yesu ndani ya roho yangu na kwa akili yangu tu. Mtakatifu msimamizi wa kikanisa changu alikuwa Mwokozi juu ya Mlima wa Mizeituni. Wakati mwingine nilichoshwa sana kwa kusubiri kibali cha wazazi wangu ambacho kilichukua muda mrefu. Hata hivyo, ninataka kuendelea na ujenzi wangu kwa kigezo kwamba ninaishi. Tangu mwaka 1924 tayari nilikuwa najisikia tama ya kujitoa sadaka kwa ajili ya

Sura ya Pili

Mwokozi. Hisia za wasiwasi dhidi ya masumbufu na kunyimwa kibali na wazazi wangu zilikuwa kubwa. Walinisikitikia lakini shauku yangu kwa Mwokozi ilikuwa kubwa zaidi. Nilihisi kana kwamba „tulikuwa wawili”. Nilizuiliwa kukutana na Masista, jambo hili lilifanya mahangaiko yangu kuwa makubwa zaidi. Potelea mbali, sikuweza kulisema hilo kwa wazazi wangu. Vilevile kulikuwa na kishawishi na mashambulizi ya adui yangu mkuu ambaye bado alisema nami kwamba sifai vya kutosha kujiunga na shirika lolote kwa sababu siwezi kufanya kazi yoyote. Jibu langu lilikuwa: Fanya kazi, taabika, na okoa roho. Katika umri wa miaka 15, niliweleza kwa dukuduku wazazi wangu kuhusu vitu ambavyo nilinyanyaswa kwavyo. Sikuelewa vitu vingi katika maisha yangu na shukrani kwa

hilo niliweza kushinda vishawishi vingi kwa urahisi zaidi, bila ya kujua madhara ambayo yangeweza kutokea.⁴⁹



Mkandidati Helena Hoffman

Helena alifanya kazi kama mkandidati kwenye hospitali ya huko Rozdzen. Alifanya kwa ujuzi mkubwa kwa kujitoa na kwa upole.

Aliutoa msaada wake kwa wagonjwa kama mche wa huduma kwa Kristo. Si kama kwa kushona tu, kama watu

Sura ya Pili

walivyozoea kusema kuhusu yeye, lakini vile vile kwa huduma iwayo yote kwa wagonjwa. Wagonjwa ndio ambao hasa aliwapenda; na alijifunza mapendo hayo kwa Mtakatifu Theresa wa Mtoto Yesu, ambaye alikuwa na mawasiliano naye ya ndani.

Mwanzoni mwa mwaka 1928, wakati ambapo Mama mkuu alipotembelea huko Rozdzien, Helena alipokea kola ya upostulanti ambayo ilikuwa na maana kwamba amepiga hatua nyingine ya kuelekea usista. Kwa hali hii aliweza kuwa jirani zaidi na Mwokozi kama “Kipenzi chake” na kwa hiyo alitambua uwepo wake katika Shirika la Masista wa Maria Imakulata. Tangu wakati ule, alitoa hata sadaka kubwa zaidi, jitihada na mateso, kwa ajili ya Yesu na Maria.

Katikati ya mwezi Machi mwaka 1928, Helena alikwenda Wroclaw. Huko kwenye nyumba ya shirika aliendelea na malezi yake ya upostulanti. Alifurahi sana kwenda pale, alirudia maneno aliyoyasikia moyoni mwake: “Yesu anaita kwa ajili ya sadaka yangu”. Utaratibu wa kawaida wa mapokezi ya kuwa mpostulanti Shirikani yalifanyika 17.03.1928. Alifurahi sana kuwa mpostulanti. Furaha yake ilingusa kila mtu – wapostulanti wengine na masista. Mtakatifu Theresa alikuwa akimpatia Helena mwongozo wa jinsi ya kufanya mazoezi katika fadhila na kumweleza kwa niaba ya yule ambaye twamsumbukia na namna ya kuwa mkamilifu.

Helena, akiwa mtawa, alipenda kuwa mtakatifu. Alitaka kufikia lengo lake kwa kuwa mwaminifu katika Kanisa, kuwaombea mapadre, Kanisa zima, Papa, pamoja na Shirika – viongozi na masista wengine; kwa kusali kwa ajili ya wadhambi na roho zinazoteseka toharani; kwa kuwa msaada kwa watu wengine. Kwa namna hii alikuwa akiokoa roho kwa ajili Kristo. Kila kitu alichofanya, alifanya kadiri ya maneno ya Kristo: “Kama ulivyomtendea mmoja wa hao

Sura ya Pili

ndugu zangu walio wadogo, ulinitendea mimi”⁵⁰ na kanuni ya Mtakatifu Augustino: “Enenda kwa kupitia mwanadamu na utamfikia Mungu”⁵¹.



Kwenye Chekechea

Wakati ule, kwa Helena, ubinadamu tayari ulikuwa ukimaanisha kuwa ni njia ya Kanisa. Alijua kwamba kwa kumsaidia mtu anamtumikia Kristo anayeishi ndani ya kila mmoja wetu. Alijua kwamba angeweza kufikia lengo lake kwa kusali kwa makini na kwa kutoa sadaka. Kwa hiyo aliyafanya majukumu yake ya kila siku bila dosari. Kristo Mteswa alikuwa ni mfano wake bora. Alitambua kuwa ndiye aliyekuwa akimwita, akimwalika kwa sadaka. Kwa hiyo, maisha yake yote yalikuwa kama jibu kwamba alikuwa akijitoa kikamilifu kwa Kristo anayeishi katika Kanisa lake. Hata wakati akiwa mgonjwa alikuwa tayari

⁵⁰ Mt. 25:31-46; Biblia Takatifu, Jimbo la Iringa, 1997

⁵¹ Cit. : Komentarz sw. Tomasza z Akwinu, kaplana do Ewangelii sw. Jana.,: Liturgia Godzin. Codzienna modlitwa Ludu Bozego, t. III, Pollattinum 1984, s. 255

Sura ya Pili

kwa sala na kazi ngumu. Kanuni ya Kibenediktini: “Ora et labora” – “Sala na Kazi” haikuwa kanuni aliyoifahamu.

Utakatifu unapatikana kwa sadaka. Hakuna mwafaka kwenye njia ya kuelekea utakatifu, taswira ya Mungu lazima ilindwe katika moyo wa mtu wakati wote; uovu, dhambi, lazima vife ili kwamba mtu mpya, akizitumikia amri za Mungu, aweze kuzaliwa. Na kwa kweli, ni dhambi ambayo ndiyo adui wa utakatifu – maendeleo ya kiroho ya binadamu. Dhambi hujumuisha ubinadamu katika uwepo wa “mafumbo ya maovu”

Mtakatifu Theresa aliye mdogo, ambaye aliyaongoza maisha ya kiroho ya Helena, alimtaka kutii mwungamishi wake na wakuu wake kila siku; vile vile kutunza kwa siri kila jambo ambalo amemweleza au kumwonesha, vinginevyo, Helena ataweza kupoteza fadhila zote alizopewa. Kwa kweli maisha yote ya Sista Dulcissima yalikuwa ni utambuzi wa tamaa ya kuwa katika uficho, hata hivyo, aliwapatia wengine furaha.

Katika nyaraka za ofisi ya Makamu Mkuu wa Shirika, Sista Honorata, twaweza kusoma:

Mkandidati Helena alikuwa mgonjwa kwenye Nyumba Mama kwa muda fulani. Tulipokuwa tunafikiri kuwa hewa ya mjini huenda inamdhuru, tuliempeleka katika kijiji chetu huko Henrykow. Pale alirudia afya yake na alikuwa akiwasaidia masista kufanya kazi za nyumbani. Kwa sababu ya utayari wake na upole wake, masista wote walimpenda. 3.01.1929 alikuwa mgonjwa mno. Mganga mpya toka Henrykow, Daktari Krischker, alithibitisha kuwa ana uvimbe kwenye ubongo. Alipoteza fahamu. Fahamu zilimrudia siku ya pili lakini kwa kitambo tu. Daktari alisema kwamba hakuna uwezekano wa yeye kurudia afya yake, kwa hiyo tulimtaarifu mama yake. Mamaye alikuja haraka sana lakini Sista Dulcissima hakuwa na ufahamu wowote kuhusu ujio huo. Daktari hakusaidia chochote na alisitisha matibabu. Lakini

Sura ya Pili

mara mkandidati huyu alirudia afya yake, jambo ambalo lilikuwa ni furaha kubwa kwa masista⁵².

Katika siku za mwanzoni za ugonjwa wa Helena, Masista waligundua kwa mara ya kwanza kuwa alikuwa akizungumza na Mtakatifu Theresa. Ingawa hili lilitokea pasipo ufahamu wake, waliweza kufuatilia majadiliano yake yasiyokuwa ya kawaida. Kwanza Helena alimkaribisha Mtakatifu huyu kwa maneno: “Tumsifu Yesu Kristo”. Kisha aliyaelekea mang’umuzi yake yote kwa Theresa, kama mtoto. Mtakatifu huyu alikuwa anacheza naye kama mama na mtoto wake mdogo. Kisha pamoja walikuwa wanakuwa wanatengeneza bustani; walireki, kusia, kupanda na kumwagilia maji. Mtakatifu Theresa alikuwa akimfundisha Helena sala mbalimbali. Wakati mwingine Helena alikuwa akimchekesha na kumfurahisha Mtakatifu Theresa pia na kumwuliza kwa unyenyekevu kama mtoto kuhusu mambo mbalimbali. Wakati wa ukaaji wa Helena huko Henrykow, masista vilevile walitambua kuwa hata alipokuwa na afya, alikuwa akizungumza naye usingizini⁵³.

Kwenye Mkesha wa Noeli mwaka 1928 Helena akijisikia dhaifu, kwa hiyo alibaki kitandani.3.01.1929 alikuwa mgonjwa sana na inawezekana kwa sababu ya uvimbe wa ubongo. Wakati ule mafua yalienea Henrykow kote, lakini Masista walidai kwamba hayo yalikuwa ni mambo ya kawaida na kwamba Helena asingeweza kuathiriwa na ugonjwa huo, tokana na Masista waliowatunza wagonjwa walisema kuwa inawezekana hiyo ilikuwa ni kwa sababu ya utata wa uvimbe wa ubongo. Sababu pekee ya ugonjwa wa Helena ni mapenzi ya Mungu. Mara mama yake alikuja. Alilia kumwona mtoto wake mgonjwa lakini alipata kitulizo kuwaona Masita

⁵² O. J. SCHWETER, *Oblubienica krzyza*, 27

⁵³ Ibid.,

Sura ya Pili

wakimtunza binti yake kwa uangalifu mkubwa. Aliketi pamoja nao kando ya kitanda cha Helena. Usiku wa tarehe tano kuamkia sita ya mwezi Januari, Helena aliamka na mara aliona kitu ambacho si cha kawaida. Kati ya saa sita na robo mpaka saa saba alipiga yowe usingizini: “The..., The..., Theresa, unakuja kwangu!” Helena alikuwa ni mwenye furaha na aliongea na Mtakatifu Theresa. Mara moja Mama yake waliwaita ili wawe mashuhuda wa mazungumzo kati ya mgonjwa Helena na Mtakatifu Theresa. Ilikuwa si namna ya kawaida kwa kuwa Helena hakuweza kuongea kawaida, hivyo aliwasiliana na watu kwa kalamu na kipande cha karatasi. Usiku uliofuata Mtakatifu Theresa alitokea tena. Baada ya kupokea Mpako wa Wagonjwa, Helena alipata nafuu⁵⁴. Siku chache baadaye hatari ya kifo ilitoweka moja kwa moja, hata mama yake aliweza kurudi nyumbani.

Kabla Helena hajarudi kwenye Nyumba Mama ya Shirika huko Wroclaw mwishoni mwa mwezi Marchi 1929, Daktari Klein aliyekuwa anaongoza hospitali ya Masista wa Mtakatifu Elizabeth huko Ziebice, alimpatia Helena cheti cha matibabu kifuatacho:

Bi Helena Hoffmann, anayekaa kwa muda kwenye nyumba ya Masista wa Maria Imakulata huko Henrykow, alipimwa muda mfupi na sikuona mabadiliko yoyote ya tiba dhidi ya upungufu mdogo wa damu. Matokeo ya majaribio ya kipimo maalum cha Kifua kikuu nayo yameonesha hasi. Kwa hiyo namchukulia Bi Helena kuwa ni mwenye afya na hana hatari yoyote ya kifo⁵⁵.

Hati hii ilithibitishwa na Daktari Klein.

Kuhusu ukaaji wa Helena kwa mara ya pili kwenye Nyumba Mama, Sista Honorata, Mama Mkuu Msaidizi, jumuya hati iliyotaja hapo juu, alisema:

⁵⁴ cf. Ibid., 28

⁵⁵ O. J. SCHWETER., *Oblubienica krzyza*, 28

Sura ya Pili

Helena bado ana maumivu ya kichwa baada ya kurudi kwake. Siku moja, mara tu baada ya kurudi, alianguaka kwenye ngazi na kutumia muda wa siku kadhaa akilala kitandani bila ya kujitambua. Siku hizo alizungumza na Mtakatifu Theresa vile vile. Maongezi yalichukua takribani saa moja. Alipata nafuu haraka baada ya ajali na masista walimpenda kwa ustadi na upole wake⁵⁶.

Nyakati zingine maumivu ya kichwa yalikuwa makubwa sana kiasi cha kumpelekea kupoteza fahamu.

Masista walihofu sana kuhusu jambo hilo, sababu sherehe za kupata nguo za kitawa na kuingia novisiati zingekua si za uhakika. Mganga binafsi, Daktari Pusch, alishauri kumpeleka mgonjwa kwenye Hospitali ya Chuo Kikuu ya Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu ili akapimwe na Profesa Mann. Helena pamoja na mkandidati mwingine walipelekwa kule na Mlezi wa Wakandidati, Sista Katharina. Baada ya kuwapima wakandidati wote, profesa alimwambia Sista Katharina: “Msischana huyu (Helena) anaweza kupata shela lakini huyu mwingine mwondoeni”. Kipimo cha mionzi (X-ray) kimeonesha uvimbe wa ubongo ambao inawezekana ulisababishwa na muwasho wa ubongo ambao Helena alikuwa nao huko Henrykow. Daktari alisema: “Na apewe shela. Hakika, maumivu ya kichwa hayatakoma, lakini hii si sababu ya yeye kuondoka”⁵⁷. Helena alipokea matazamio ya kuwa na maumivu makali ya kichwa ya mara kwa mara. Bila kujali hayo, alitaka kupangiwa majukumu ya kazi za kitawa.

Mnamo tarehe 23.10.1929, Siku ya Mkombozi, Helena alipata sare ya kitawa na jina la Maria Dulcissima. Siku ya Mtakatifu msimamizi wake ilikuwa tarehe 16 Septemba. Namba yake ya kitawa aliyopokea ilikuwa ni 987. Aliandika: Shukrani kwa huruma ya Mungu na msaada

⁵⁶ O. J. SCHWETER., *Oblubienica krzyza*, 29

⁵⁷ Ibid.,

Sura ya Pili

wake vilevile kwa wakubwa, baada ya mwaka mmoja wa upostulanti, niliruhusiwa kupewa shela. Siku ya utawa ilikuwa ni siku maalum, iliyojaa neema. Nilifurahi sana. Ulikuwa ni uamuzi wangu mwenyewe binafsi kwamba nilikwenda utawani, kuuvunja utashi wangu mwenyewe na kujijeredisha mwenyewe. Nilitaka kuyachukulia maisha ya kitawa kama jema kuu na kuishi kufuatana na imani hiyo⁵⁸.

Sista Dulcissima pamoja na wanovisi wengine wawili, walipelekwa Nysa, ambapo tangu mwaka 1925, Nyumba ya Unovisi ya Masista wa Maria Imakulata iliwekwa. Mlezi wa wanovisi pale alikuwa Sista Pacyfika Schimke, ambaye hata kabla yake alikuwa na kazi hiyo huko Wroclaw. Nafasi ya ubaba wa kiroho wa wanovisi pamoja na Shirika zima, tangu mwaka 1925 ilishikiliwa na Wincenty Groeger toka Lubsko, mlezi wa awali, na tangu mwaka 1934 kama paroko huko Bardo ya Lek, karibu na Warta.

**Helena Hoffmann –
Mnovisi**



⁵⁸ cf. Ibid., 30



**Sista Dulcissima Mnovisi wakati wa unovisi,
akuwa na wanovisi wengine.**

Kwa uwazi na kwa unyenyekevu Sista Dulcissima aliandika kuhusu muda wake wa unovisi:

Mwaka wa kwanza wa unovisi ulikuwa kama mnyororo wa tajriba inayoendelea: niliona karaha dhidi ya masista wengine, kwa kuishi nao; nilijihisi ukavu, kutokuwa na uwezo wa kutenda haraka na ukaidi katika maisha ya sala. Sikuwa na uwezo wa kumwambia yeyote kuhusu hili. Sikupenda kulalamika wala kutafuta faraja. Nilishughulika na hali hiyo mimi mwenyewe. Suluhisho la mfungo wangu mwishoni mwa mwaka wa kwanza ulikuwa ni kuendelea kufanyia mazoezi katika maisha yangu kila kitu nilichojifunza wakati wa mwaka mmoja wa unovisi: okoa roho kwa ajili ya Mwokozi na kuwa mtakatifu kwa majukumu ya kawaida⁵⁹.

Katika mwaka wa kwanza wa Unovisi, kwenye kitabu Kikanisa Changu iliandikwa, ambapo Sista Dulcissima aliandika katika Utii kwa Mlezi wake wa

⁵⁹ O. J. SCHWETER., *Oblubienica krzyza*, 32

Sura ya Pili

Unovisi: Si nyakati zote mwingi wa muhtasari wake ulieleweka kwa wasomaji. Hata hivyo, waliruhusu kuelewa ukweli kwamba Sista Dulcissima mwanzoni mwa safari yake ya kiroho alipata mfano bora wa kufuata. Muhutasari wa asili ulioandikwa na Sista Dulcissima – akitiwa moyo na Sista Theresa, ulichomwa moto. Kulitokea kutoelewana kati ya Sista Mlezi na Sista Dulcissima. Sista Dulcissima alidai kwamba asingeweza kuchoma moto muhtasari kwa vile hajapokea ushauri wowote kutoka kwa Mtakatifu Theresa kuhusu jambo hilo⁶⁰.

Maneno ya Sista Mlezi: “Uko kwenye njia potofu” yalimfanya Sista Dulcissima kuhuzunika, kwa kuwa aliamini kwamba Mtakatifu Theresa hakika alizungumza naye. Vilevile alimwuliza mwungamishi wake kuhusu jambo hilo muhimu la maisha yake ya kiroho. Alikuwa akijaribu kuituliza akili yake, akiendelea kusema kwamba njia yake aliyokuwa ikiipita haikuwa ya uongo; kwa kufuatana na ndoto zake, ni lazima awe mtulivu na mkimya – hii ingeweza kuwa nzuri tu ikiwa mmoja ameitwa kwa kusali na kutolea sadaka, na hakuona haja yoyote ya kulieleza hili kwa mtu yeyote.

Baada ya mwaka mmoja mnovisi Dulcissima alipelekwa Nyumba Mama. Alitakiwa kuwatumza wasichana na kwa uangalifu kutazama maisha yao ya kidini na kimaadili. Aliiogopa huduma hiyo kwa sababu alijihisi dhaifu sana. Alishikwa na wazo: Mimi sifai. Kwa hiyo, hakuwa na uhakika na kutojitegemea kwa alichokuwa anafanya. Yeye mwenyewe alisema kuhusu hilo: “Nina furaha kuu kwamba ninaweza kufanya kitu fulani, lakini kwa woga tokana na elimu yangu ya kujitegemea na kwa kuwaogopa watu nilipokuwa nakwenda Nyumba Mama. Lakini pamoja na hayo yote kwa uradhi kabisa nilifanya kila

⁶⁰ cf. J. SWASTEK, *Zyjac dla innych*, 118

Sura ya Pili

kitu kwa utii. Nilifanya kwa jitihada yangu yote ili kwamba nilisionyeshe kwa yeyote nini kilikuwa kinatokea ndani ya roho na akili yangu.(..) Nilirudi Nysa, kwenye unovisi, na pale Mwokozi bado alinifanya nitaabike kwa ugonjwa wangu.

Mnamo tarehe 21.03.1931 nilimwomba Mwokozi kutimiza mapenzi na nia zake kwangu hata kama ingelimaanisha ni kwa ugonjwa na mateso. Nilitolea sadaka kila kitu kwa ajili ya Shirika. Siku tatu baadaye, mnamo tarehe 25 Machi, Siku ya Kupashwa Habari Bikira Maria, nililala nikiwa mgonjwa mahututi. Nilikuwa na mshtuko wa moyo na nilipewa sakramenti ya mpako ya wagonjwa⁶¹.

Kadiri ya taarifa ya walioshuhudia kwa macho, Sista Dulcissima walikua kwenye hali tete, ambapo Mganga binafsi, Daktari Skrobek, hakuweza kuthibitisha maumivu kama alivyodai kuwa ilikuwa ni pigo la umanyeto. Kwenye Jumapili ya Pasaka ya tarehe 5.04.1931, Sista Dulcissima alirudia uhai baada ya siku kumi za kutokuwa na fahamu na machafuko. Hili lilitokea kabla ya alasiri, wakati Masista Arimathea, Pacyfika, na Lazaria walipoona kitu kisichokuwa cha kawaida. Sista Dulcissima alikipa jina “Ndoto” ambayo kwayo Mtakatifu Theresa alimtokea na kuzungumza naye. Kuhusu tukio lile Sista Arimathea alisema: Kwa vile leo ni siku ya Kwanza ya Pasaka, Mungu mwema anampatia furaha kubwa, kwamba anaweza kuwaona malaika⁶².

Kinyume cha Sista Arimathea, Sista Pacyfika hakuamini uhalisia wa tajimba wa mtawa huyu na kudai kwamba lazima wawe makini sana kuhusu Helena kwa sababu ni mgonjwa. Bi Kalinka, daktari toka Nysa, aliitwa kumpima. Daktari alielezea hali ya mchango wa mafigo.

⁶¹ O. J. SCHWETER, *Oblubienica krzyza*, 33

⁶² O. J. SCHWETER., *Oblubienica krzyza*, 33

Sura ya Pili

Mgonjwa alipelekwa Berlin kwa uchunguzi. Kama alivyoshauri Sista Mlezi, walijaribu kumlazimisha Helena kwa upasuaji wa kichwa. Utoboaji wa fuvu uliamuliwa kufanyika siku iliyofuata. Sista Dulcissima, hata hivyo, alimwea, kama alivyoshauri Sista Theresa kuwa asikubali upasuaji na kwa hiyo arudi Nysa⁶³.

Mnamo tarehe 10.08.1931 Sista Dulcissima alirudi Nysa, ambapo kwa furaha alijiunga na mazoezi ya unovisi. Muda wote alikuwa mkweli na mnyenyekevu kwa wakuu wake na kwa Masista alikuwa mnyenyekevu na kuwa wazi kufanya kazi na kusali.

Mnamo tarehe 12.08.1931 alikuwa na pigo lingine ambalo lilisababisha kupotelewa na fahamu. Lilidumu hadi tarehe 19 Agosti. Muda huo alipokea tena mpako ya wagonjwa. Ikiwa imedhania kuwa angeweza kufa, Sista Dulcissima aliulizwa endapo katika hatari ya kufa, angependa kufunga nadhiri kwa masharti. Alikubali mara moja na kwa sauti aliweka nadhari zake za ufukara, usafi wa moyo, utii na upendo wa daima. Ya mwisho aliiongeza mwenyewe kama alivyoyaona maisha mazima ya utawa ushiriki hai katika mapendo kamili. Kisha afya yake iliboreka kidogo.

Siku Noel ya mwaka 1931, licha ya maumivu makali, alikuwa ni mtu mwenye furaha na mchangamfu. Alikuwa mtu wa kwanza unovisini na alitaka kutoa mfano mizuri. Januari mwaka 1932, Padre Joseph Schweter alikuwa akitoa mafungo huko Nysa. Sista Dulcissima alianza kushiriki kwa makini kufuata mafungo, lakini kwa bahati mbaya, hakuweza kumaliza mafungo. Shambulio jingine la uvimbe wa mafungo na hali nyingine mbaya zilimfanya awe kitandani. Mashambulizi yakaanza kumrudia.

⁶³ Ibid., 34

Sura ya Pili

Marchi 1932, baada ya shambulio lingine, Sista Dulcissima alipoteza fahamu kwa siku tatu. Mara, baada ya kitambo kifupi, Sista Dulcissima alipokuwa uisingizini alikuwa anaongea na Mtakatifu Theresa, na mara Sista Lazaria aliingia. “Niliutikisa mwili wake, sista Lazaria aliandika - mpaka alipopata fahamu, na nikamuuliza kilikuwa ni nini kile alichokuwa anazungumza nacho. Alikaa kimya. Alikuwa amekaa kitandani na baada ya kusita alikiri: Theresa Mdogo alikuwapo hapa na amesema tayari ninaweza kula, kunywa na kuamka. Ilikuwa ni kwa mara ya kwanza kwa Sista Dulcissima kuniambia juu ya maono yake, kwa kuongezea, kwa njia ya asili kabisa. Nilimwita Sista Mlezi wa wanovisi na Sista Dulcissima alirudia maneno yale yale naye akiwepo. Sasa Helena alikuwa anakunywa bila shida. Sista Mlezi wa wanovisi alimruhusu kuamka. Alijivisha mwenyewe na hata kula kidogo kachumbari ya mboga. Kwa siku tatu za msukosuko na kupoteza fahamu hakuweza kunywa hata kimiminika. Japo alikuwa na maumivu makali ya kichwa baada ya kuumwa, “hakuna hata mmoja aliyelitazama hilo na kilielewa” - alilalamika⁶⁴.

Kwa ombi la Sista Dulcissima, Sista Lazaria akawa muuguzi wake. Naye Sista Lazaria vilevile ameacha maneno machache:

Wakati wa uangalizi wa usiku, wakati akiwa mnovisi, nilikuwa nikimsikiliza katika ndoto zake akiongea na Mtakatifu Theresa kwa dakika chache. Hata hivyo, nilikuwa muwazi kwa Sista Mlezi na nilimwambia kila kitu pamoja na fikra zangu. Wakati Sista Dulcissima alipogundua hili, akawa msiri na mndani, akisema kwamba anamwogopa Sista Mlezi; kwamba asingeweza kuelewa na angeweza kumwambia amdhihirishie kila

⁶⁴ J. SWASTEK., *Zyjac dla innych*, 118

Sura ya Pili

kitu; naye asingeweza kufanya hivyo kwa kuwa hakuwa na ruhusa toka kwa Mtakatifu Theresa⁶⁵.

Kama alivyosema mwenyewe, Sista Dulcissima alipokuwa “akizama katika sala”, hakuwa akijibu chochote⁶⁶. Tangu mwaka 1932 mara nyingi alikuwa akizungumza nami: “Wakati ninapompokea Yesu katika Komunyo Takatifu, ninahisi utamu mkuu kinywani mwangu”, ingawa alipoteza hisi za uonjo mnamo mwaka 1931, aliweza tu kuhisi baridi au joto. Katika miaka miwili ya mwisho alikuwa akiniambia:

Baada ya Komunyo Takatifu ninaweza kuhisi sana moto kifuari mwangu kiasi kwamba hata sijui ni nini. Nahisi joto mno kiasi kwamba sipati pumzi; na kisha Yesu anazungumza kwa sauti kubwa ndani ya moyo wangu⁶⁷.

Wakati mmoja tulifanya hija huko Mariahilf, kikanisa kidogo cha hija katika msitu karibu na Nysa. Katika kikanisa cha Mtakatifu Rohus, Sista Dulcissima alitaka kuanzisha njia ya msalaba na kupiga magoti mbele ya picha ya Yesu iliyovikwa taji la miiba. Mimi kisha niligundua ni kwa kiasi gani sura yake ilibadilika. Hakuweza kujibu maneno yangu niliyoongea kwa sauti kubwa. Alipiga magoti kwa unyamavu na kwa kutulia, na macho yake akifumba, akazama moja kwa moja. Nilimchukua, kisha kwa mkono niliutikisa mwili wake kwa nguvu kidogo. Aliporejea, aliogopa sana, aliona aibu na kukiri kwa unyofu: “Sijui lolote. Unataka nini toka kwangu? Nilikuwa nasali tu”. Baadaye, tulipokuwa tumezoeana vya kutosha, aliniambia: Hiki ndicho nilichomaanisha – kuzama katika sala. Wakati nilipokuwa nasali mbele ya picha ya Maria Mtakatifu kwenye kikanisa cha Mariahilf, ufunuo mwingine usio wa kawaida ulitokea: Akijibu swali langu ni

⁶⁵ Ibid., 149

⁶⁶ cf. Idem

⁶⁷ Ibid., 35

Sura ya Pili

nini alichokuwa akiomba wakati wa sala alijibu: Sijasali. Nilikuwa naongea na Maria tu na sijui kingine chochote zaidi. Tafadhali, usimwambie yeyote jambo hili⁶⁸. Hata hivyo, Sista Lazaria aliona kuwa ni wajibu wake kumtaarifu Sista Mlezi kuhusu mambo haya yaliyotokea.

Mwishoni mwa unovisi alikuwa anamwandikia Yesu. Mihtasari yake ilikuwa na asili ya majadiliano ya ndani kuhusu ugonjwa wake uliokuwa unaendelea:

Ee Yesu wangu, tazama, uwezo wa macho yangu kuona unazidi kupungua sana. Kitambo kidogo sitaweza kukuandikia, lakini Ndiwe unayetaka iwe hivyo. Na niwe, Ee Yesu, na niwe roho ya ndani na si juu-juu tu. Mapendo yangu ni makubwa kwa kila tukio langu kuu. Nisamehe Yesu, na Wewe, Mama Yangu, Wa ndani, ndio – wa ndani, uwe Mwokozi wangu; ni ngumu mno kufuata njia yangu. Nipatie tafadhali ... Hapana, hata hivyo, mapenzi yako yafanyike! Ninaona aibu, ingawa nataka kumwabudu Baba Yako, ambaye ni Baba yangu vile vile. Ndio, zaidi na zaidi, je ninahitaji kuwa mtakatifu?⁶⁹

Usiku mmoja Daktari Skrobek alikuwa amekaa pembeni ya kitanda chake kwa saa nne na kumdunga sindano sita za afyuni ili kupunguza mtukutiko wa maungo. Yote ilikuwa bure! Ugonjwa ule ulikuwa zidi ya ujuzi wake na ulibaki kuwa fumbo. Sista Lazaria alikuwapo pale muda huo. Mara tu baada ya daktari kuondoka, Sista Dulcissima alitulia na kuanza kuongea na Yesu. Kisha aliongea kwa nguvu na kwa uwazi, kwa hiyo kila kitu kiliweza kusikika na kueleweka. Alikuwa akizungumza kuhusu „kikanisa chake na vifaa ndani yake”. Ilikuwa ni Alhamis, kati ya saa tano na nusu na saa sita usiku. Zaidi ya Sista Lazaria alikuwepo Mlezi wa Wanovisi na kushuhudia tukio hilo.

Pigo la mwisho kabla ya nadhiri lilitokea kati ya tarehe moja na tisa Aprili mwaka 1932. Sista Dulcissima

⁶⁸ Ibid., 36

⁶⁹ J. SWASTEK., *Zyjac dla imnych*, 118

Sura ya Pili

alimwambia muuguzi: “Sasa nitakuwa tayari kufunga nadhiri zangu takatifu; nafurahi sana kwa hilo kwa sababu nitaweza kumsaidia Yesu kuubeba Msalaba. Nadhiri zangu za mwanzo zitanifanya niwe Simoni wa Kirene”⁷⁰.

2. Kuweka nadhiri za mwanzo na muda wa nadhiri hizo

Toka tarehe tisa hadi kumi na nane Aprili mwaka 1932 Sista Dulcissima alikuwa akilala kitandani na kuhudhuria mafungo kabla ya nadhiri zake za mwanzo. Mnamo tarehe 18 Aprili, siku ya mwisho, licha ya kuwa katika hali mbaya na hali ya udhaifu kwa ujumla, aliamka na kwenda sakristia kuweka nadhiri zake za mwanzo pamoja na masista wengine. Baada ya nadhiri, kwa sababu ya afya yake, alibaki Nysa.

Sista Dulcissima siku ya Nadhiri zake za Kwanza



Mnamo mwezi Mei mwaka 1932, Katibu Mkuu wa Shirika, Sista Honorata Mazur, alishawishiwa kwamba Sista

⁷⁰ J. SWASTEK., *Zyjac dla innych*, 118

Sura ya Pili

Dulcissima anaweza kusihi mambo mengi kutoka kwa Mungu, akimwaminisha kwa nia maalum: kuthibitishwa kwa Katiba ya Shirika na Papa. Sista Dulcissima alijibu: “Ndiyo, nitamwomba Mungu”. Baada ya siku chache ugonjwa wake uliongezeka na kusababisha kupotewa na uwezo wa kuona. Sadaka ilipokelewa – “6.07.1932 Katiba iliidhinishwa huko Roma”⁷¹.

Kila siku Sista Dulcissima uwezo wake wa kuona ulizidi kudidimia; kichwa kilizidi kuchachamaa vile vile. Maumivu yalisumbua zaidi na zaidi. Mwishoni mwa mwezi Mei alipoteza kabisa uwezo wake wa kuona. Daktari katika hospitali ya Chuo Kikuu huko Wroclaw alisema kwamba upofu ulisababishwa na shinikizo la damu katika kizio cha kushoto cha ubongo wa mbele. Pale yalitokea vilevile maumivu ya ndani. Aliumizwa kwa hofu kuu; “Nini sasa kitanitokea? Nitapelekwa wapi? Siwezi kufanya chochote mimi mwenyewe, kipofu kabisa! Siwezi kufanya kazi licha ya kuwa bado ningali kijana! Nani atanisaidia sasa? Nani ataelewa hilo? Kabla ya nadhiri, mara nyingi alikuwa akisema: “Si nyumbani tu!”, na sasa aliwaza: “Mimi ni mzigo Shirikani. Nyumbani! Kuwa kijana utawani na huna uwezo wa kufanya kazi, ni nani ataelewa hili?”. Vidokezo mbalimbali vilivyofanywa na masista na wakubwa vilimfanya ataabike. Baadhi yao walielekea kumwamini Daktari Skrobek, ambaye aliielezea afya yake kama ni „mpagao”. Kulikuwa na maoni kwamba apelekwa hospitali ya wagonjwa mahututi huko Branice au aruhusiwe kurudi nyumbani.

Wakati huo, Sista Lazaria alimsikia mara nyingi alopokuwa mgonjwa mahututi jinsi Sista Dulcissima alivyokuwa akisali sala zake: “Yesu, niletee roho ambayo itanielewa na itaniamini! Unaweze kufanya kila kitu. Ni

⁷¹ J. SWASTEK., *Zyjac dla innych*, 246

Sura ya Pili

Wewe ambaye umeniletea haya yote, nayo yatoka kwako! Roho moja tu na injie”, alimwambia Sista Lazaria: “Ilimpasa Yesu ashuke chini katika njia yake ya Msalaba, nami pia ninashuka chini kwa miguu yangu sasa; kwa sababu ya woga kwamba nimechunguzwa, na kwa sababu sikuaminika na kushutumiwa kujisingizia”. Tangu mwezi Juni mwaka 1932 Sista Lazaria aliamua kuwa anakaa kando ya kitanda cha mgonjwa Sista Dulcissima⁷². Kwenye barua yake kwa Mama Mkuu wa Shirika, Sista Eulalia, tunaweza kuona mawazo ya Sista Dulcissima ambayo yameungana na dunia na Mungu⁷³.

Sista Dulcissima alikuwa na tajiriba ya mateso mbalimbali ya akili ambayo aliyaita Siku za Getsemani, lakini licha ya hayo, aliweza kujipa moyo. Alimwandikia barua shangazi yake Marta akimweleza mambo hayo⁷⁴.

18.01.1933, aliwasili katika Nyumba ya Kitawa huko Brzezine katika Odra. Akiwa pale, mateso yake pamoja na haja yake ya kutimiza mapenzi ya Mungu ilikuwa kubwa zaidi.

Akifuata mfano wa Mtakatifu Theresa, Sista Dulcissima aliyatolea mateso yake kama sadaka kwa Kanisa, kwa Papa na Mapadre, kwa Shirika, kwa wakubwa wa shirika na masista, vile vile kwa wenye dhambi wanaoteswa Toharani.

Zaidi sana, Kristo na msalaba wake alisimama katika njia ya maisha ya Sista Dulcissima. Ugonjwa katika ubongo

⁷² Taz.J. SCHWETER., *Oblubienica Krzyza*, 46

⁷³ Archiwum Siostr Maryi Niepokalanej, Katowice poz. 49

⁷⁴ Archiwum Siostr Maryi Niepokalanej, Katowice poz. 49: Katika barua hiyo Sista Dulcissima alimwomba shangazi Marta ampatie medali takatifu chache, skapulari au shajara, kadiri ya zilizokuwepo. Kila kitu kinachokutokea ghafla, lazima ukipokee kwa furaha, hata kama moyo wako unatona damu. Hivyo, mama wa kikristo lazima daima awe tayari kutii mapenzi ya Mungu.

Sura ya Pili

wake ulizidi kuongezeka, na kisha aligundua kwamba kwa ugonjwa huo anaweza kuwaambukiza wengine kutokana na huduma ya kitume. Alijielewa kwa tajiriba za mateso hasa kwa kila Ijumaa ya Kwanza ya Mwezi na kila Sikukuu ya Maria. Aliyahesabu mateso yake kama ni madogo tu. Lakini kwa Mungu hakuna mambo yaliyo madogo. Alizoea kusema kuwa hata mateso madogo yachukue kwa unyenyekevu, yana thamani sana kwa Mungu.

Mwaka wa 1933, kwa Sista Dulcissima ulikuwa ni mwaka maalum wa kuelewa utume wake, na tena kwa kina alielewa mateso ya Kristo. Sista Dulcissima litaka pia kuupokea ugonjwa wake. Kwa hiyo kila mara alipokea kila jambo kama kituo cha msalaba. Siku ya Kutukuka kwa Msalaba, aliyafananisha maisha yake na Kristo na Maria. Alimshukuru Mungu kwa wema wake aliomjalia katika maisha yake na aliomba kifo chema. Ilikuwa ni alama ya ukomavu wake. Wakati huu, alipokea madonda matakatifu ya Yesu yaliyofichika toka kwa Mungu. Hivyo, alionja kwa undani mafumbo ya mateso ya Kristo ambayo aliyaonja wakati wa kukamatwa kwake na katika Njia yake ya Msalaba.⁷⁵ Kwa hiyo, alikuwa akiitwa “Bi arusi wa Msalaba”.

⁷⁵ Martin Luther aliwaondo wafuasi katika Mapokeo. Aliacha Neno la Mungu tu. Wakristo wengi hawakuweza kusoma wakati wa Marekebisho. Aliikubali lugha mahalia katika Liturjia na Biblia. Biblia ya Pauperum, mtazamo wa ukweli wa imani katika picha. Tamaduni za Makanisa ya Kiprotestanti ni za shuruti, hawakuhitaji picha katika mandhari zao. Kwa hiyo, muda ule, Ibada ya Njia ya Msalaba ilianzishwa katika makanisa, kalvario, na picha zilikuwa vitu vya tafakari.

Sura ya Pili

3. Nadhiri za Daima na maisha endelevu ya Kitawa

Licha ya ugonjwa wake wa kudumu, wakuu wa shirika, wakigundua wito wake halisi, walimruhusu Sista Dulcissima kufunga nadhiri za daima. Akiwa karibu zaidi na Yesu katika nadhiri za milele na katika kifa, maombi yake dhidi ya roho yalikuwa ni ya pekee.



**Nadhiri za Daima
ziliwekwa siku ya Alhamisi
tarehe 18 Aprili mwaka
1933**

Sista Dulcissima amekuwa akijitayarisha kwa ajili ya siku hiyo kwa kuwa na siku kumi za mafungo ambazo zilichanganyika na maumivu makubwa ya viungo. Padre Mteule Yohane Milik alikuja Brzezic toka Katowice ili kupokea kwa maandishi shahada yake ya nadhiri. Lakini hili lilishindikana kwa kuwa Sista Dulcissima alikuwa hajitambui kwa saa 18. Katika mazingira haya Askofu Stanislaw Adamski alimwagiza padre anayewahudumia masista toka Brzezic Oblate Blandzi kupokea nadhiri⁷⁶.

⁷⁶ D. SALIK., *Siostra Maria Dulcissima Hoffmann oblubienica krzyza*, 18

Sura ya Pili

Sista Dulcissima alifanya mafungo yake ya kiroho kabla ya nadhiri akiwa chumbani kwake, akiongozwa na Padre Blandzi. Mama Mkuu alitangaza ujio wake kwa ajili ya sherehe ya nadhiri za daima. Hata hivyo, jambo moja maalum la muhimu lilimfanya asiweze kufika. Makamu wake, Sista Honorata, alifika badala yake. Toka Katowice alikuja Mkuu wa Provinsi, Mama Dolorosa Andrzejczak alimkumbusha maneno ya nadhiri Sista Dulcissima ambaye karibu alikuwa kipofu kabisa. Kwa kweli ulikuwa ni muda wa kimungu kwa Sista Dulcissima ambaye wakati wa maadhimisho alisimama akiegemea gongo la kutembelea. Aliandika maneno ya nadhiri yeye mwenyewe, ilimchukua siku kumi na nne kuyaandika⁷⁷.

Mara nyingi Sista Dulcissima alikuwa akizungumzia kifo chake mara kwa mara. Madhumuni yake yalikuwa ni:

Kutengeneza hatua ya mwisho pamoja na Yesu na Maria, Kuwa na Yesu kwa njia ya Maria na kukaa naye milele, Kuwa na moyo wa kumwendea Yesu, Kumshukuru Mungu wa mema yake kwa yote yaliyopita na kumwomba kwa umilele ulio mwema. Kutopoteza fadhila, kwa dunia yote⁷⁸.

Aliyachukua mateso yake kwa saburi kubwa. Aliuchukua Msalaba huo akiunganisha na mateso Yesu Kristo, akiwa mtii kabisa kwa mapenzi ya Mungu. Akiwa amekaa upenuni mwa kitanda cha mgonjwa Sista Dulcissima, Sista Klotylda Kaczmarczyk alitambua kuwa alikuwa akiongea na mtu fulani kimya kimya. Masista wengine walimwambia Sista Klotylda kwamba Sista Theresa wa Mtoto Yesu alikuwa akimjia Sista Dulcissima⁷⁹. Ilifuatia kwamba ujio wa Sista Theresa ulijulikana kwa masista wengine.

⁷⁷ O. J. SHWETER., *Oblubienica krzyza*, 91-92

⁷⁸ J. SWASTEK., *Zyjac dla innych*, 121

⁷⁹ Archives of the Sisters of Mary in Wraclaw, t. III, 1930-1950

Sura ya Pili

Mnamo Septemba mwaka 1935 Sista Dulcissima aliandika barua yake ya kuaga kwa wazazi wake na kaka zake vile vile kwa baba yake mlezi Henryk⁸⁰.

⁸⁰ J. SWASTEK, *Zyjac dla innych*, 250

SURA YA TATU

Kuutafuta Utakatifu

1. Mvuto wa Mtakatifu Theresa wa Mtoto Yesu kwa Maisha ya Kiroho ya Sista Dulcissima

Ili kuyaelewa maisha ya Sista Dulcissima, ni muhimu kwanza kuyatazama maisha ya Mtakatifu Theresa. Kama inavyojulikana, Sista Dulcissima akiwa bado mtoto, aliiona medali takatifu ikiwa na picha ya Mtakatifu Theresa. Tangu muda ule alijiweka chini ya maongozi wa Mtakatifu Theresa.

Theresa Martin – kama jina lake halisi lilivyokuwa – alizaliwa tarehe 2.01.1873 huko Alencon. Wakati alipokuwa na umri wa miaka minne na nusu, baada ya kifo cha mama yake, baba yake alihamia Lisiuex. Alikuwa akiwa akipendwa na baba yake na dada zake wanne⁸¹. Mnamo tarehe 29.04.1923, alitangazwa Mwenyeheri na Papa Pius XI, na alitangazwa Mtakatifu tarehe 23.05.1925⁸². Alileta kitu kipya katika maisha ya mwanadamu mwishoni mwa karne ya 19. Maisha yake yanatoa mwongozo wa namna gani tunaweza kuishi; yanaeleza kuwa kila hali ni lazima itakatifuzwe. Mnamo tarehe 19.10.1997 Papa Yohane Paulo

⁸¹ Taz. Theresa Martin akiwa na umri wa miaka kumi na tano, kwa ruhusa ya Kanisa iliyotolewa na Papa Leo XIII alijiunga na Wakarmeli huko Lisiuex. Alipokea jina la Theresa wa Mtoto Yesu wa Uso Mtakatifu. Alikuwa ni Msakristia katika nyumba ya utawa. Kazi yake ilikuwa ni kutengeneza hostia. Alikuwa akizichora vile vile. Akiwa mgonjwa wa Kifua Kikuu, aliugua sana. Kisha alichora picha ya Yesu akiwa anabisha hodi kwenye mlango wa moyo. Alijulikana kama “Njia Ndogo ya Utoto wa Mungu”. Alikufa tarehe 30 Septemba mwaka 1897.

⁸² Taz. Autobiografii sw. Teresy od Dzieciatka Jezus, Lisiuex 1957, s. 227-229

II alimtunukia heshima Mtakatifu Theresa wa Mtoto Yesu kuwa Mwalimu wa Kanisa.⁸³

Sista Dulcissima hakuiona medali ya Mtakatifu Theresa kwa kudra za Mungu, bali Mtakatifu Theresa wa Lisiuex alikuwa na mchango wa pekee katika maisha ya kiroho ya Sista Dulcissima. Baadaye aliandika: Siwezi kuwa utawani sasa⁸⁴. Aliyaelewa vizuri sana mawazo ya Mtakatifu Theresa. Huduma yake wa Kitume ilikuwa kuteswa na kubeba msalaba. Mtakatifu Theresa alimfundisha Sista Dulcissima katika maisha yake yote kukua katika upendo wa Mungu na wa wanadamu. Alimfundisha namna ya kuishi, na ‘Si kupata ukuu kwa Mungu’. Alikuwa akimwonyesha karaha ya dhambi katika hali ya kimulimuli cha tufe jeusi ambalo alitakiwa kulishika, au katika hali ya bustani ya maua yenye nyoka ambao walionesha vichwa vyao na ndimi zao.

Tunaweza kuichambua njia ya maisha ya utakatifu ya Sista Dulcissima kua kuyaangalia maisha ya Mt. Theresa. Mfanano wa tabia yao unaweza kuonekana sana katika hali ya unyofu wa mtoto mdogo. Sista Dulcissima alizoea kusema kwa maneno ya Mtakatifu Theresa: “Mimi ni mpira mdogo, mimi si kitu”.

Ushauri wa Mtakatifu Theresa, ukiwa unaonyeshwa katika picha, ulimfanya Sista Dulcissima awe na furaha. Theresa alimwonesha Sista Dulcissima bahari yenye samaki. Bahari ilimaanisha Kanisa, na samaki ni roho za watu. Mvuvi alikuwa ni Mwokozi mwenyewe na fadhila zake. Wakati mwingine alimwonesha bahari kubwa yenye maji mazuri ya mawaridi juu ya uso wake. Mtakatifu Theresa alisema: “Kuna mizizi ya neema, na samaki

⁸³ Taz. Ni heshima inayotolewa na Kanisa Katoliki kwa baadhi ya Watakatifu, ambao wanaheshimika kwa maisha yao ya Utakatifu, walioshika sheria na utaratibu za kawaida za tabia ya Kiroho na Kiteolojia.

⁸⁴ Taz. J. SCHWETER, *Oblubienica krzyza*, 24

wadogo ni watu, “samaki wa Kristo”. Ndege wazuri waliokuwa wakitua kwenye mkono wa Mtakatifu Theresa zilikuwa ni roho zilizookolewa kwa maombezi yake. Wakati ule Theresa alimwonesha mlelewa wake njia nyembamba sana ambayo ni mtu mmoja tu angeweza kutembea. Theresa alikuwa akitembea kwanza, Helena kama mtoto, alikuwa akimfuatia kwenye kilindi kilichogubikwa kwa moshi, makorongo yenye giza. Theresa alielezea: “Hili ni giza, dunia iliyovurugika”. Mpaka mwisho wa maisha yake, Helena alikuwa akijihisi kama mtoto mwenye umri mdogo mbele ya Mtakatifu Theresa. Vyovyote vile, hili lilikuwa ni lengo la yale “mafumbo ya ufunuo” ya Mtakatifu Theresa: kumwongoza Helena katika maisha ya kiroho ya utoto, na hivyo kumwongoza katika utakatifu wa kweli⁸⁵.


Maisha ya kiroho ya Sista Dulcissima yalikuwa na „ukubwa wa Utatu Mtakatifu”. Alijitakatifuza kabisa mwenyewe kwa Utatu Mtakatifu, akiomba zawadi ya wito katika Jumapili ya Utatu Mtakatifu. Maisha yake yalitiwa msukumo na Roho Mtakatifu, Maria na Mtakatifu Theresa. Katika maisha yake alifuata njia ya Ukweli, ina maana njia ya Kristo. “Yeye anionaye Mimi, amemwona Baba”. Sista Dulcissima alielewa kuwa Kristo ni msingi na waamini wake ni mawe hai. Kwa hiyo Sista Dulcissima mwenyewe alikuwa akijenga nyumba yake ya imani juu ya mwamba ambao ni Kristo. Tabia halisi na za kawaida za utakatifu wa Mtakatifu

Theresa na Sista Dulcissima ni: unyenyekevu wa kuwa kama mtoto, mapendo motomoto kwa Yesu na Maria, moyo wa shauku kuhusu roho, ujasiri wa kustaajibisha katika mateso, na utayari wa kuwa msaada kwa watu wengine vile vile na moyo uliojazwa saburi.

Sista Dulcissima, na Sista Lazaria, na Mt. Theresa

⁸⁵ Taz. J. SCHWETER, *Oblubienica krzyza*, 24

wa Mtoto Yesu



Katika maisha yake, Sista Dulcissima aliiga mfano wa Mtakatifu Theresa wa Utoto Mtakatifu, ambaye alimwonyesha njia fupi iendayo kwa Mungu⁸⁶. Ujasiri wake katika mateso uliosababishwa na upendo wake kumwelekea Mungu na jirani ni ushahidi mkubwa na mfano kwa Wakristo wa leo.

2. Mateso na Sadaka

Maisha ya kitume ya Sista Dulcissima yalikuwa ni mateso na kubeba Msalaba. Alianza kuugua wakati akiwa bado mtawa mdogo. Kwa bahati nzuri wakuu wake waliona kuwa hakuna sababu ya kuogopa kuwa na Wanashirika wagonjwa kwa sababu wao ni kama baraka. Mfano wa

⁸⁶ A. PLACZEK, *Swieta Teresa od Dzieciatka Jezus nauczycielka nowej drogi swietosci*, W: Brzeski Parafianin 4 (1996) 5, s. 3

kweli wa kuiga wa mateso ya Sista Dulcissima ni mateso ya Kristo. Alijua kuwa ni Yeye (Kristo) aliyemwalika kutoa sadaka. Kwa hiyo maisha yake yote yalikuwa ni jibu lisilo na mwisho alilompa Kristo katika maisha ya Kanisa. Hivyo, maisha yake yalikuwa na mtazamo wa kikanisa. Alikuwa wazi daima kwa milango ya heri za Mungu. Hata alipokuwa mgonjwa sana alikuwa tayari kusali na kufanya kazi.

Ni kwamba alipokea maisha ya mateso ya mwili tu kama utii kwa mapenzi ya Mungu, lakini vile vile alikuwa tayari kuteswa zaidi hasa pale alipoombwa kusali kwa nia maalum, au pale ambapo yeye mwenyewe alipoona umuhimu wa kuomba kwa fadhila fulani. Mwanzoni kulikuwa na nyakati ambazo alilalamika: “Mtu analalamika na kuona shauku – ni kwa muda gani haya yote yatadumu?” Kwa kuhisi, alidhani kwamba ulikuwa ni ugonjwa wa kupita, inawezekana ukaisha mara na usitokee tena. Hata hivyo, ugonjwa haukwisha, na tena alikuwa bado alijinyenyekeza na kuwa mtii kwa Mungu, akisema: “Mungu na aniruhusu kujitoa sadaka, bila ya upumbavu ule wa ukaidi wa kibinadamu”⁸⁷.

Ugonjwa uliendelea. Wakati wa usiku Sista Dulcissima alikuwa akipiga magoti kando ya kitanda chake au kulala sakafuni kwenye kona ya chumba. Alisali na kulia. Alimshukuru Mungu kwa kuteseka: “Mwokozi ni Mwema. Nimepokea zawadi mpya. Ulimi wangu ni mzito, na kichwa changu pia. Lakini si kitu kwangu”⁸⁸.

Kadiri ugonjwa wa Sista Dulcissima ulivyokuwa unaendelea, Sista Lazaria alimpeleka kwa daktari bingwa wa mfumo wa mfumo wa fahamu. Alimfanyia utafiti kwa undani na aligundua kuna kupooza kwa neva za upande wa kushoto katika mwili wake wote. Alimwanzishia matibabu lakini hayakuonesha matokeo yaliyotarajiwa. Moja kati ya

⁸⁷ ASMN, Katowice, poz.50

⁸⁸ Ibid.,

mikono yake, na sehemu ndogo ya kichwa havikuwa na hisia vile vile. Baada ya majuma manne masista walikwenda kwa daktari mwingine, ambaye kwa njia ya kifaa maalum, aligundua uvimbe wa ubongo. Uvimbe ulishinikiza neva nyingi kwa nguvu tofauti ambazo zilisababisha mabadiliko ya hali ya Sista mara kwa mara⁸⁹.

Utambuzi wa ugonjwa ulithibitishwa: Uvimbe kwenye upande wa kushoto wa kizio cha ubongo, umejaa majimaji. Mbali na mateso hayo, alipoteza kabisa kumbukumbu na uwezo wa kuongea. Ni baada tu ya muda mrefu wa kufikiri, ndipo aliweza kuelewa ni nini kilikuwa kinasemwa juu yake. Licha ya maumivu mfululizo, kwa tabu sana alilala kitandani. Kama vile kila mara alivyoweza kufanya kazi yoyote ya ndani, ndivyo alivyofanya hata kazi nzito kwa bidii. Miongoni mwa mambo makubwa matatu yaliyomkabili hadi auone ugonjwa wa kifua kikuu kama zawadi kwa mkubwa wake ni: Mnamo Desemba mwaka 1932 afya yake ilikuwa mbaya sana kiasi kwamba alipoteza fahamu katika mashambulizi⁹⁰.

Kila hatua ilikuwa ni ngumu kwake, alikuwa na hisia kwamba angeweza kuanguka mara. Hakuweza kuwasiliana kwa maneno, hivyo aliongea kwa ishara. Kila mara alisema na Mwokozi katika sala zake ili achukue kila kitu kilicho chake. Licha ya kuwa ukweli ni kwamba alikuwa na homa kali kila mara na maumivu makali kichwani, alikuwa na maono ya kinabii yaliyoungana na vita vijavyo. Lakini muda huo huo aliwahakikishia wananchi wa Brzezic kwamba, hakuna chochote ambacho wanapaswa kukiogopa kwa kuwa hata msukosuko wa vita unaweza kupita tu.

Mwishoni mwa maisha yake, makovu ya Yesu Msulubiwa - alama maalum ya mapendo ya Mungu, yalianza kutokea katika mikono, miguu na katika ubavu wa

⁸⁹ J. SCHWETER, *Oblubienica krzyza*, 47

⁹⁰ J. SCHWETER, *Oblubienica krzyza*, 61

SURA YA TATU

mwili wake. Katika “Chronik Mutterhaus der Marien Schwester Breslau 1914-1950”, toka kwenye ofisi ya nyaraka za kumbukumbu za Masista wa Maria Immakulata katika Nyumba ya Provinsi huko Wroclaw, kuna muhtasari kuhusu maisha ya Sista Dulcissima ambayo yanathibitisha uwazi wake kamili kwa mapenzi ya Mungu⁹¹.

Sista Dulcissima aliyachukua mateso pasipo kulalamika: aliweza hata kuyafurahia. Alijitoa kabisa kwa mapenzi ya Mungu. Akiwa tayari ameteswa vikali kwa ugonjwa wake, alikuwa amezoea kushuka chini ambako alizoea kupiga magoti mbele ya sanamu ya Mtakatifu Yosefu na kumwabudu Yesu kwa kupitia dirisha wazi kwenye kikanisa cha watawa.

Wakati wa Kwaresma, Sista Dulcissima alitoa matoleo maalum kwa mapenzi ya Mungu kwa kupokea kupooza kwa ulimi na mkono wake wa kushoto. Mwezi uliofuata alisali kwa ajili ya Mapadre, wokovu wa dunia, na kuzidishiwa utakatifu mabruda na watawa⁹².

Pale afya ilipomruhusu, Sista Dulcissima pamoja na Sista Lazaria waliwatembelea wagonjwa katika nyumba zao, wakiwapa heshima na kuwatajulia hali.15.12.1933, Sista Lazaria aliteuliwa kama Mama Mkubwa wa nyumba ya Brzezic lakini aliendelea kumhudumia Sista Dulcissima⁹³.

Siku hadi siku hali ya Sista Dulcissima bado ilizidi kuwa mbaya. Usiku na mchana kila siku alikuwa na mfululizo wa maumivu makali ya mtikisiko wa maungo na mchango. Katika usingizi wake alikuwa akiongoea kuhusu kuja mara kwa madhulumu na umwagaji damu: “Salini na jitoeni vya kutosha. Janga litakuja toka Berlin na litasambaa hadi

⁹¹ Taz. ASMN, Katowice, poz. 50

⁹² Taz. D. SALIK, *Siostra Maria Dulcissima Hoffmann oblubienica krzyza*, 16

⁹³ Taz. J. COP, *Patrzmy na swietych, ktorzy w wierze nam przewodnicza i ja, udoskonalaja*, 43

Silesia. Linaweza kutujia hapa Poland. Lakini msioCOPE, mko katika mikono ya Mungu”⁹⁴.

08.07.1934 alimwomba Mkubwa atolee Misa na Novena kwa ajili ya ulinzi wa nyumba ya Masista wa Maria Immakulata kwa maana alitabiri kuhusu nyakati ngumu zijazo. Mnamo mwezi Novemba, mwaka ule ule, alisema: Ghasia kuu itatokea. Ndio, yowe la binadamu litakuwa kubwa zaidi ya la wanyama. Katika fujo hizo watu watauana, kutakuwapo na uadui mkubwa kati ya mtu na mtu. Aliwasikia mapadre wakilalama wakiwa wanachukuliwa kwenda kwenye magereza ya maadui. Nisaidie, tusaidie, tuokoe, tulettee msaada, okoa roho zetu. Alisikia kilio cha nguvu vile vile, na alifikiri kwamba alikuwa ni Yesu aliyefungiwa kwenye tabernakulo, kama vile ilivyokuwa kwa Yerusalem zamani za kale. Kwa hiyo alitumia muda mwingi sana kanisani. Ulikuwa ni muda mzuri wa kukusanya hazina ya kiroho – alinena kwa dhati”⁹⁵.

Sista Dulcissima aliyachukua mabegani mwake mateso ya watu wengine kama Yesu alivyofanya. Ni rahisi kwa mtu kutoa uhai wake kwa ajili ya mwingine lakini ni vigumu mno kuyachukua mateso yao. Ni kiwango cha juu sana cha tabia za Kikristo dhidi ya mateso. Zaidi na zaidi kujinyonga kulikuwa ni jambo la kawaida kwa watu waliokuwa na hofu kuu ya mateso. Hawakuogopa kifo – waliogopa mateso. Mtazamo wa Sista Dulcissima kuhusu mateso ulikuwa ni wa thamani kuu na wa aina yake kinyumecha ya mtazamo wa amali dhana hii.

Maneno yasemayo: “Bwana, aliishi na aliteswa – kwa ajili yaw engine” yanaweza kurejewa kwa Sista Dulcissima. Kwake Yeye Mungu, upendo wa namna hiyo ni upendo kamili. Kila teso jipya aliloteswa Sista Dulcissima, alilipokea kama zawadi aliyopewa na Mwokozi. Aliyaita

⁹⁴ J. SCHWETER, *Oblubienica Krzyza*, 83

⁹⁵ Taz. Ibid., 85-86

mateso yake kuwa ni “madogo” kulinganisha na mateso ya watu yanayopita kiasi. Alimaanisha kutoipoteza ile fadhili ya Mungu, ambayo ni urafiki wake, ili kwamba asiweze kuwa mbali naye. Akiwa mnyenyekevu na mtii kwa Mungu, aliweza kusema: “Mungu na aniruhusu kujitoa mwenyewe sadaka, bila ya ule upumbavu wa ukaidi wa kibinadamu”⁹⁶.

Upekee wa Msalaba ni kwamba, Mwana wa Mungu alitundikwa juu yake. Na mapendo ya Mungu yana nguvu sana kuliko dhambi. Sista Dulcissima alikwenda kilindini mwa fumbo la upendo wa mateso ya Kristo. Miongoni mwa vitu vingine alivyoandika: „Ee Yesu, nienende katika njia yangu ya Msalaba ili kwamba upendo wangu kwako, kwa Maria na kwa jirani uzidi sana kila siku. Ujaze moyo wangu kwa furaha takatifu, ili tu kwamba baadaye nifurahi”⁹⁷. Sista Dulcissima alijitoka kabisa mwenyewe kwa Mungu. Roho yake ilitukuka wakati wa matatizo makubwa.

Gongo alilokuwa akitumia kutembelea lilikuwa zito; mara nyingi alijipiga nalo katika hali yake iliyofanana na ya mtoto na kujiita kwa majina yake. Mtakatifu Theresa alilitolea maoni akisema: “Huu ni msalaba wako ambao Yesu amekupatia kwa hiyo uuheshimu. Gongo hili litakuwa na maana sana baada kifo chako”. Maneno hayo yalisikika katika hali ya watoto. Kwa unyofu alijiambia mwenyewe: “Yesu amekutoa wewe kwangu. Ni lazima nikuheshimu”. Aliibusu fimbo ya msalaba kila mara na kuitumia kama kitu cha kupendeza.

Dunia ambayo ilikuwa ikienda mbali na Mungu iliifanya roho ya Sista Dulcissima kuwa na huzuni. Alikuwa na wazo la utume ili kuwa sadaka itonayo haki ya Mungu ili mkono wa Mungu wenye kuadhibu uliupige ubinadamu kupita kiasi. Muda ule aliandika tafakari zake juu ya Njia ya Msalaba. Tangu Ijumaa, mnamo mwaka 1936, alianza

⁹⁶ ASMN, Katowice, poz. 50

⁹⁷ D. SALIK., *Siostra Maria Dulcissima*, 17

maisha mapya ya fumbo la Msalaba. “Katika mtazamo wa kiroho alikuwa akiisukuma njia yake kupitia kwenye kundi la askari kuelekea msalabani kwenye kilele cha Golgotha kwa Yesu, ili awe jirani naye zaidi. Sista Lazaria alimwona Sista Dulcissima akichukua mkono wake wa kulia kana kwamba anauruhusu kupigiliwa mishumari msalabani, akiwa anaendelea kulalamika: “Abba, Abba, Magister, Mater Dolorosa”⁹⁸. Njia hiyo ya Msalaba ilirudiwa kila Ijumaa mpaka mwisho wa safari yake ndefu duniani. Nyakati nyingine, aliteseka sana, nyakati nyingine – kiasi, lakini alilichukua kila moja na kuomba mapendo zaidi ya Yesu.

3. Kifo – Utimilifu katika Yesu Kristo

Katika miaka ya mwisho ya maisha yake, Sista Dulcissima alikuwa akijitayarisha kwa kifo na kila mara aliongea kuhusu kifo. Alitamani sana kukutana na Kristo mchumba wake uso kwa uso. Mwaka 1936 ulikuwa ni mwaka wa mateso makuu kwa Sista Dulcissima na hakuna njia yoyote ya kawaida iliyomsaidia kupunguza maumivu. Mwezi Aprili ulikuwa ni muda wake wa mwisho alioongea na Masita, wakati walipokuwa huko Brzeznie wakati wa mafungo matakatifu.

Tangu tarehe mosi ya Mei mwaka huo huo, Sista Dulcissima alikuwa katika hali ya kukosa nguvu, si ya kutembea wala ya kujisogeza. Na wakati wa juma lake la mwisho, aliwaita walei kando ya kitanda chake, akimwita kila mmoja kwa jina lake. Mnamo tarehe 12 Mei alipata Mpako wa Wagonjwa na kupokea Komunyo Takatifu kwa mara ya mwisho. – Alisema tena: Ee Yesu, Wewe u ndani yangu, nami ni ndani yako. Wewe ni kila kitu – Mimi si kitu. Yesu, ningependa kuwa Sadaka mpya ya damu, na niwe hivyo. Sisi sote ni roho za sadaka. Kwa hiyo hatuna

⁹⁸ J. SCHWETER., *Oblubienica krzyza*, 113

budi kukufuata kuelekea Golgotha. Nimeishi duniani bila ya kujijua, kwa kuwa yalikuwa ni mapenzi ya Mungu. Bila kujijua ninatoweka mbali nawe na hamtaona mwujiza wowote. Daima Yesu alikuwa upande wangu. Ninakwenda nyumbani⁹⁹.

Alisema kwa ukweli kabisa: “Nitakufa; hamtaona mwujiza wangu sasa”. Mwujiza, katika hali ya mazungumzo ya maneno, haukuelezwa wakati wa kifo chake, hata hivyo, sala zisizo na idadi zimesikilizwa katika hali isiyo ya kawaida¹⁰⁰. Yeyote aliyeweza kumwona Sista Dulcissima katika siku na masaa ya mwisho ya uhai wake, lazima aliweza kuona kufanana kwake na Mwokozi akiteswa msalabani.


Wakati wa uhai wake, wakati akikaribia kufa, alikuwa akimwambia Sista Lazaria: Katika mikono yako hii, nitakufa. Utakuwa ni wewe ambaye utayafumba macho yangu. Na ilitokea hivyo. Mnamo siku ya Jumapili tarehe 17 mwezi Mei, Sista Dulcissima alimwambia Sista Lazaria: Yesu daima yuko upande wangu. Hakuweza kupokea Komunyo kwa sababu ya kushindwa kumeza, hata hivyo daima aliungana na Mwokozi. Baada ya chakula cha jioni, alisema: Je wewe humwoni Malaika mlinzi? Hupendi tu kuniambia kuwa unamwona. Tazama; amesimama hapa, nyuma ya pazia ya kitanda. Tayari ameshanionesha njia nzuri. Ni nzuri sana. Baadaye kidogog alisema ghafla: Nimekwisha zungumza na mama, ninakwenda nyumbani. Alipokuwa anasema hivyo, mkono wake ulinyanyuliwa. Wakati Sista Lazaria aliposema: huwezi kufa sasa, alijibu: Nyamaza. Kisha aliendelea kusali kwa sauti kubwa kama desturi hadi usiku wa manane¹⁰¹. “Mnamo usiku wa manane, Sista Dulcissima aliita kwa Kipolandi: ‘Mama

⁹⁹ Taz. J. SWASTEK., *Zyjac dla innych*, 250

¹⁰⁰ Taz. J. SCHWETER., *Oblubienica Krzyza*, 113

¹⁰¹ Taz. J. SWASTEK., *Zyjac dla innych*, 122

Mkubwa, haraka, haraka!’ Lakini baadaye akapata usingizi. Mnamo tarehe 18 Mei, Sista Lazaria akiwa amekuja chumbani, aligundua kwamba Sista Dulcissima alipumua kwa shida. Mara moja alimpatia dawa zake za moyo. Kisha lilitokea jasho jembamba na uso ulio dhaifu. Padre Blandzi alimpatia maondolea ya jumla ya dhambi kwa mara nyingine – Mpaka wa Wagonjwa. Kwa pumzi ya utulivu kabisa, midomo iliyokwajuka, bila msukosuko, bila mashindano: ilikuwa ni kwa ukimya kabisa “alikuwa anakufa”. Kama maisha yake yalivyokuwa ya ukimya na ya usiri, ndivyo na ulivyokuwa umauti wake. Muda ule ule wakati kengele zikiwa zinalia kwa ajili ya sala ya Malaika wa Bwana, pumzi yake alizidi kuwa dhaifu zaidi na zaidi mpaka mapigo ya moyo wake yaliposimama mnamo saa 11:30”¹⁰²



¹⁰² Ibid., 123

Taarifa za Kifo cha Sista Dulcissima

Kifo kizuri, cha kirafiki na cha maelezo mazuri usoni mwake – wenye kutabasam na fahari. Dhihirisho la sura yake, mara tu baada ya kifo, lilikuwa kama tabasamu la kirafiki la mtoto mdogo. Lilibaki hivyo mpaka jeneza lilipofungwa baada ya siku nne. Kulikuwa na hisia za harufu

ya



pekee ya maua kando ya jeneza lake, kana kwamba ni Balsam. Mara nyingi Sista Dulcissima alimwambia Sista Lazaria: Utaona, jioni hii nitalala kitandani mwangu na asubuhi sitaamka tena. Rafiki zangu watakuja upesi. Jambo hili lilikuja kuwa kweli neno kwa neno. Moja ya mambo kama ya mtoto aliyoyatamani ni kuingia katika umilele muda ule ule ambapo kengele zilikuwa zikilia kwa Malaika wa Bwana. Alipendelea sana kuimba wimbo wa ‘Nitapenda kukusifu, Ee Bikira, kwa sauti yangu ya mwisho, nikisimama mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, muda ambao kengele zinalia kwa Malaika wa Bwana! Ave Maria! Na hivi ndivyo ilivyomtokea.

Katika miaka yake ya mwisho alizoea kusema:

SURA YA TATU

**kwa Yesu. Kwa hiyo kila mmoja na afurahi.
Wewe, Sista Lazaria, wapatie kahawa na keki.**



Alitaka kupendeza baada ya kifo chake ili kwamba asiwepo yeyote atakayeogopeshwa naye. Na hivyo ndivyo ilivyotokea. Alikuwa mzuri kama mtoto alalaye kwa

SURA YA TATU

utulivu. Ilipojulikana kuwa amefariki, watoto wa shule walipiga yowe mitaani: **“Sista mgonjwa, aliyekuwa kama Theresa Neumann wa Konnersreuth, amefariki”**. Watu kwenye shule za Kipolandi na Kijerumani walikuwa wakiliongelea hilo. Watu toka pande zote walikuwa wanakuja kwa makundi kumwona akiwa amekufa. Mwili wake uliguswa kwa punje za rosary, picha takatifu, medali na vipande vya kanzu yake ya kitawa na kilemba vilikatwakatwa. Akina mama waliwapeleka watoto wao kubusu mikono yake kwa mara ya mwisho. “Tayari yuko mbinguni” – watu walimwongelea, licha ya kwamba walimtambua kwa kuona tu.

Licha ya tufani na joto, hakuna mabadiliko yaliyoonekana kwenye mwili mfu wa Sista Dulcissima. Uso na mikono yake ilikuwa bado mizuri na viungo vyote vya mwili wake vilinyumbuka. Hata watu wazima nao, walikuja kumwona na kubusu mikono yake bila woga. “Alikuwa ni mwanamke shahidi. Alikuwa mtakatifu” – walimwongelea. Watu wa kawaida walikuwa wanaleta maua na mishumaa kwenye jeneza lake kila siku. Paroko, Padre Borzucki alimwambia Sista Lazaria asiweke mapambo ya maombolezo.

Alisema: “Hata hivyo alikuwa mtoto, na hivyo, nguo za maombolezo zisivaliwe”. Kwa hiyo, masista walipamba kila kitu kwa rangi nyeupe. Nyumba nzima ilijazwa kwa utulivu na furaha. Wakati huo huo Suffragan Askofu Brombaszcz toka Katowice alikuwa na ziara parokiani. Kutokana na tukio hilo, kila kitu kilipambwa kisherehe: kanisa, kikanisa kidogo cha Masista na nyumba; vyote vilipambwa kwa mashada ya maua. Siku ya mazishi, yaani tarehe 22 Mei, Ijumaa baada ya Sikukuu ya Kupaa Bwana, ilikuwa ni kama maandamano ya harusi. Kwenye maandamano ya mazishi, wanovisi wapya wanne waliopokelewa, mara baada ya kupokea vilemba, walionekana kama wasindikizaji wa bibi harusi kwenye

harusi ya mbinguni. “Kulikuwa na maandiko yaliyotengenezwa kwa kasha la mbao juu ya sanduku: “Magnifikat” kwa upande mmoja, na “Te Deum” kwa upande mwingine. Wanachama wa Shirika la Maria walikuwa wakiimba “Magnifikat” – Moyo wangu wamtukuza Bwana. Mkuu wa shule ya Kipolandi, Bi Kubica, aliwapeleka watoto wa Komunyo ya kwanza wakiwa wamevalia nguo nyeupe wakiwa na maua ya yungiyungi na mataji wadogo vichwani mwao”¹⁰³.

Mazishi ya Sista Dulcissima

Baadhi ya kumbukumbu zenye uhusiano wa maisha ya Sista Dulcissima, kama vile msalaba, sanamu ndogo ya Mtoto Yesu, sanamu ndogo ya Mama Yetu Malkia, vinara vya mishumaa, picha zilizochorwa za siku ya kupewa kilemba au sanamu ya Mtakatifu Yosefu vimebakia kwenye nyumba ya watawa ya Masista wa Maria Immakulata huko Brzezie.

Sanamu ndogo ya Mtoto Yesu



¹⁰³ Ibid, 116-117

SURA YA TATU



**Sanamu ya Mtakatifu
Yosefu**

Sanamu ya Bikira Mari



SURAY A NNE

Roho Yake I-Kati Yetu

Sista Dulcissima alikuja kutukuzwa kwa hiari baada ya kufa. Kaburi lake daima lilipambwa kwa mishumaa na maua chungu nzima. Watu wengi walimweleza kwa siri matatizo yao. Idadi ya ushuhuda wa fadhila kwa wale waliohitaji toka kwa Mungu kupitia maombezi ya Sista Dulcissima yamekuwa yakiongezeka. Watu bado wanalitembelea kaburi lake hadi sasa. Idadi ya watu wanaozulu kaburi lake iliongezeka kwa kasi wakati wa Vita vya Pili vya Dunia. Watu walisali kwenye kaburi lake. Walikuwa wakichukua udongo toka kwenye kaburi ili kwamba waweze kuulinda milango yao dhidi ya maadui – Wajerumani na Warusi. Watoto waliuhifadhi udongo wa kaburi la Sista Dulcissima hata kwenye mikebe ya kalamu zao za risasi. Waliyatunza hata majani ya maua yaliyomea kwenye kaburi vile vile. Na hata leo, bado wanafanya vivyo hivyo. Udongo toka kwenye kaburi lake ulichukuliwa hata na Wajerumani waliokuwa wakimiliki Brzezic; hat Warusi pia walifanya hivyo. Walitaka kurudi kwa furaha kwenye familia zao. Kwenye kaburi lake, walifika watu wa jamii za kila namna, sio tu wa kutoka Brzezic, bali hata wa kutoka vijiji na miji jirani.

Sura ya nne

Hili lilitokea kwa sababu kwa Dulcissima unaweza kuja na kila kitu – Ninakwenda kwake kama niendavyo kwa mama – anasema Bi Joanna¹⁰⁴.

Naazima uchukue udongo kidogo toka kwenye kaburi. Unafanya kazi kama ngao. Masista wanalazimika kuleta ndoo chache za udongo kaburini kila juma kwa sababu bado unapotea – ana lsema ajuza mmoja¹⁰⁵.

Siku hizi watu wanao kiasi kidogo kidogo, na wanauweka katika magari yao. Wanaweka mabongemabonge ya udongo kwenye masanduku yao, na kujisikia kuwa wako salama, hasa wanapokwenda ng'ambo (ugenini).

Huko Brzezic anaitwa kwa kifupi “Dulcizma”. Watu wenye matatizo mbalimbali wanamjia; wakimwomba kupata muujiza, hasa wa afya. Sista Dulcissima hupata afya toka kwa Mungu. Hivi ndivyo watu wa nchi hii wanavyofikiri. Anayachukuwa magonjwa yao mabegani mwake na kwa hiyo wanapona. “Hiyo si muujiza ...” – wanasema wakazi wa Brzezic. Sista Dulcissima amekuwa akiwasaidia kwa zaidi ya miaka 60 sasa.

Katika kaburi la Sista Dulcissima “kuna nuru muda wote” au “mishumaa inayowaka” – watu wa hapo wanasema. Waendao kanisani hupitia pale baada ya Misa na kusali. Watoto, vijana, familia nzima wanakuja. Chochote unachomuomba Sista Dulcissima, daima utapata – anasema Maria Sochiera. Alikuwa ni mtakatifu tayari wakati wa uhai wake.¹⁰⁶

¹⁰⁴ Taz. J. DOMINIK, Swieta z Brzezic. Cudowna Ziemia. “*Gazeta wyborcza*” 1999 [z 2. IV]

¹⁰⁵ Ibid

¹⁰⁶ Taz. Interview with Maria Sochiera, Brzezic of. May 19 1998.

Sura ya nne

Maneno yanayoandikwa kwenye makaburi kwa kawaida yanahusiana na maisha ya watu waliokufa na vilevile yanaeleza ushuhuda wa imani yao katika hija yao ya hapa duniani. Kwenye kaburi la Sista Dulcissima kuna msalaba, kama ilivyo kwenye makaburi ya masista, na juu ya msalaba kuna picha yake pamoja na maandishi yafuatayo: “Msipokuwa kama watoto wadogo, hamwezi kuingia katika Ufalme wa Mungu. – Mhesh. S. M. Dulcissima Hoffmann Sista Wetu wa Shirika la Masista wa Maria Imakulata anapumzika hapa katika Mungu”.

Mpaka mwisho wa maisha yake, Sista Dulcissima alikuwa jasiri mwaminifu kwa misioni ambazo Mungu amemwagiza. Kwa neno moja – alikuwa mwaminifu kwa wito wake mpaka kufa. Alikuwa ni ushuhuda dhahiri wa ushidi wa Kristo dhidi ya dhambi, kifo na Shetani. Kwa namna hii aliingia katika historia ya utakatifu katika ardhi ya Silesia.

Kwa maisha yake ya ujasiri, anaitua sisi kuamini kuwa Mungu ni upendo. Usiogope mateso, msalaba, kwa kuwa msalaba ni njia ya mwokovu. Inaweza kusemwa kwamba “watakatifu wanarudi tena”. Kwa kuwa watakatifu humuiga Kristo, kwa namna hii yaliyatoa maisha yao maelekeo fulani. Na ndivyo alivyokuwa Sista Dulcissima – “Mtumishi wa Mungu”.

Poland kuna idadi kubwa ya wanaokiunga mkono kiti cha enzi cha Mungu. Kanisa linamwona Sista Dulcissima kuwa ni miongoni mwa watu hao. Kwa Sista Dulcissima, Kristo ni mfano na thamini ya juu sana. Kwa thamani hii kuu, ambayo ni Mungu, tunaweza tu kumjia kwa kupiga goti, kama Sista Dulcissima alivyofanya wakati wa uhai wake na hasa wakati wa ugonjwa wake.

Sura ya nne

Sista Dulcissima hakutaka kuwa wa pekee. Na ukweli huu si wa pekee. Kamwe hakulalamika. Alitabasamu kwa kila picha aliyopiga, kitu ambacho hakikuwa rahisi tokana na ugonjwa wake endelevu, na kisha alama za madonda matakatifu ya Bwana katika mikono, miguu na ubavu. Alimwachia Mungu aongoze maisha yake. Kama tuonavyo katika mateso yake aliyoyaonja, tunaweza kufikia hitimisho kwamba kwa kujitweza kwake aliyakubali mateso, akiyafananisha na Mateso na Ufufuko wa Kristo. Njia ya maisha yake ni ya akili tambuzi na ya kubadilika, katika nyanja zote za maisha, yakihusishwa na mateso.

Kwa mtu kuyapokea mateso yake kunawezekana pale tu anapomuiga Kristo, kwa upande mwingine, kuiga huko hakutoweki kirahisi, isipokuwa wakati mwingine ni baada ya jitihada za ndani dhidi ya mtu mwenyewe na Mungu. Kwa mtu kuyaweka mapenzi yake chini ya Mungu ni mafanikio ya mwisho ya jitihada hii.

Sista Dulcissima hakuyapokea mateso yake kwa sababu ya kujipatia utakatifu tu mwenyewe, bali alilifanya hilo kwa ajili ya watu, Kanisa, Shirika, na kwa namna ya pekee kwa ajili ya mapadre.

Wakati mmoja, Mkuu wa shule huko Brzezic, Bi Kubica, aliongea na Sista Dulcissima: “Kama tungekuwa na watoto, mume wangu angalikuwa na nguvu na furaha kubwa zaidi. Akiwa mgonjwa wa Kifua Kikuu, mara nyingi alipoteza matumaini na kusema: “Kwa nini naishi katika ulimwengu huu?” Sista Dulcissima aliyasikiliza kwa makini maneno hayo na kisha alisema: “Nitamwomba sana Yesu, na Yesu atakupatia mototo. Utaona!” Majadiliano hayo yalifanyika mwezi Mei mwaka 1935 na mnamo Agosti alimwambia tena mwanamke yule yule: “Usiogope. Mtoto atatoka kwa Yesu na hatagua. Huruhusiwi kufanya chochote, wala hata kumsikiliza daktari”. Mnamo 7/6/1936,

Sura ya nne

mtoto wa kiume mwenye afya alizaliwa bila ya matata yoyote¹⁰⁷.

Wakati fulani Paroko padre Borzucki toka Brzezie alimwomba Sista Dulcissima kusali kwa ajili ya kaka yake ambaye alikuwa mgonjwa wa akili. Baada ya majuma machache, kaka yake huyo ambaye alikuwa na ugonjwa usioponyeka alipona kabisa na kuruhusiwa kutoka kwenye hospitali ya vichaa. Ugonjwa huo haukuweza kumrudia tena. Iliithibitishwa na madaktari wa Mtakatifu Jadwiga - Daktari Switala na Daktari Wolny.

Sala nyingi sana zinajibiwa tokana na maombezi ya Sista Dulcissima. Hili linatokea hata siku hizi. Kaburi la Sista Dulcissima linaonekana ni ukumbusho wa kumbukumbu isiyo ya kawaida ya vizazi vilivyobarikiwa vya waamini wa Brzezie na jumuiya mahalia. Kwa zaidi ya miaka 60 wamekuwa wakisali kwa Sista Dulcissima na kumwomba kama daraja kwa Mungu ili kupata fadhila kadha wa kadha.

Sista Dulcissima alitabiri vita lakini alisema na jumuiya ya Brzezie: “Msikimbie hapa. Hakuna chochote kitakachowapata huku Brzezie. Mtataabika kwa njaa tu”. Na hakika, kijiji hakikuharibiwa licha ya mapambano pande zote.

Njaa iliingia, wakati ambapo kulikuwa na Wanovisi vijana katika nyumba ya utawa. Sista Lazaria, ambaye alikuwa ni mlezi na rafiki wa Sista Dulcissima, alilia akikaribia kabisa kukata tama: ‘Dulcissima, lakini uliahidi kuwa utatutunza!’ Baada ya muda mfupi, kengele ya mlango ililia. Jirani, Gertruda Twardowska, ambaye alikuwa mtoto mara nyingi alikuwa akitembelea nyumba ya masista, aliukimbilia mlango. Kulikuwa na mtu mgeni amesimama

¹⁰⁷ Taz. J. SCHWETER, *Oblubienica krzyza*, 122

Sura ya nne

barazani na mikate mikubwa miwili. Aliwaambia: ‘Nimeambiwa niilete hapa’. ‘Niliichukua ile mikate’ – Gertruda alisema – ‘na kukimbia kwa Sista. Na tuliporudi hakukuwa na mtu yeyote mlangoni’¹⁰⁸.

“Nilikuwa mgonjwa na alikuwa akiniombea akiwa ameshika rozari yake mikononi” – anasema Bi. Viktoria Cieslik toka Brzezic. “Alipokuwa hawezi kuinuka, aliniita na kunipatia punje za rozari hii. Aliahidi kwamba atakuwa ananisaidia maisha yangu yote. Na ndivyo inavyotendeka” – alisema akiwa katika hali ya hisia.

Kwa ujumla kila mmoja aliyefika Brzezic alielekeza hatua za miguu yake kwenye kaburi la Sista Dulcissima. Watu wanasali wakitiririkwa machoni mwao; wanaleta maua, wanawasha mishumaa na kusali sala kwa muda mrefu. Ukumbusho wa maisha ya kustaa jabisha ya mtawa huyu kijana katika ardhi ya Silesia bado unaendelea kuwepo. Si kwamba heshima kwa Sista Dulcissima inatolewa na wakaazi wa Brzezic au marafiki na ndugu zake Sista Dulcissima tu; bali ni pamoja na Masista wote wa Shirika la Masista wa Maria Immakulata ambao miongoni mwao upo ushawishi kwamba Sista Dulcissima ni mtu mtakatifu. Masista wengi wamefanikiwa kutokana na maombezi yake. Masista ambao binafsi walimfahamu au kusikia habari zake, walimtolea ushuhuda.

Baba Mtakatifu Yohane Paulo II akiwa amesimama kwa muda mrefu kwenye picha ya Sista Dulcissima akimweleza kwa faragha Sista Paulina Szczepanczyk – Mama Mkuu toka Brzezic mnamo tarehe 26 Agosti mwaka 1998 alisema: “Ninamtakia heri! Yeye ni kazi ya Mungu!”

¹⁰⁸ ¹⁰⁸. Taz. F. KUCHARCZAK, “Nie chciała być nadzwyczajna. I to jest nadzwyczajne”, *Gosc Niedzielny*, IV 1999

Sura ya nne

Mchango mkubwa kwa kutangazwa Sista Dulcissima kuwa Mwenyeheri ni upendo wa desturi ya sala. Heshima hii imekuwa badi inaendelea. Inaelezwa kwa kuwasha mishumaa kwenye kaburi lake, kusali kwa muda mrefu kando ya kaburi lake, na kuchukua udongo toka kandokando ya kaburi. Watu wanaendelea bado kuleta maua kaburini wakati wengine wanachukua petali za maua hayo ili kuziweka kwenye vitabu vyao vya sala, mikoba yao, au hata kuzishonea kwenye majaketi au vizibao vyao. Watu wanaotembelea kaburi lake hawakumfahamu na hawamfahamu yeye mwenyewe binafsi, hawajui chochote kuhusu maisha yake, wameweza tu kuamini katika nguvu ya shani hii inayoitwa Sista Dulcissima.

Kaburi la Sista Dulcissima linatunzwa vizuri. Ana wanaompenda sana miongoni mwa vijana na watu wazima ambao wanasali kando ya kaburi lake, wakiyakabidhi matatizo yao kwa Mungu. Ukumbusho wa maisha yake ya ajabu na ushawishi wa nguvu ya maombezi yake vitaendelea kuwepo.

Mnamo mwaka 1994 Sinodi ya Maaskofu kuhusu Maisha ya Wakfu iliyofanyika Roma, iliorodhesha namna za maisha yaliyotolewa kwa Mungu. Sinodi vilevile ilibainisha hitaji la kuuonyesha ulimwengu sampuli za maisha ya kimonaki ambayo yanachagizwa kwenye kumbukumbu za watu wa Mungu. Mfano wa maisha hayo yaliyosabiliwa kwa Mungu huko Salesia ni ile kumbukumbu isiyoyana ya kawaida ya maisha ya kitawa ya Sista Dulcissima.

Sura ya nne



2/5/1998, Mkuu wa Provisi Sista Dionizja Patalas aliwasilisha kwa Askofu Mkuu wa Poland ombi la kuanzishwa kwa mchakato wa kumtangaza Sista Dulcissima kuwa Mwenyeheri.



Sura ya nne

**Kuanza kwa Mchakato wa kumtangaza Sista Dulcissima
kuwa Mwenyeheri**



PRYMAS POLSKI

Varsavia, il 17 marzo 1998

N. 913/98/P.

Kuria Metropolitalna w Katowicach
Wpł. 25. 03. 1998
Nr
Ant.

Eccellenza Reverendissima,

Con la pregiata lettera del 11 febbraio 1998, (VH V-4314/98) Eccellenza Vostra, secondo le Norme della Congregazione per le Cause dei Santi, (nr.lla), ha chiesto l'opinione della Conferenza Episcopale Polacca per istruire il processo di Beatificazione e Canonizzazione della Suor Dulcissima (nel secolo Helena Joanna Hoffman), professa della Congregazione di Maria Immacolate, deceduta nell'opinione di santità il 18 maggio 1935 a Brzezine sulla fiume Odra.

Dato che si tratta di una persona conosciuta in Slesia e meritata per la Chiesa in questa regione, i Vescovi Polacchi radunati nella sua Sessione Plenaria a Varsavia il 11-12 marzo 1998, condividono l'idea di organizzare il detto processo diocesano ed hanno espresso il loro voto positivo al riguardo.

Di Vostra Eccellenza devomo in Cristo e Maria

† Józef Card. Glomp
Presidente della Conferenza Episcopale
Primate di Polonia

A Sua Eccellenza Rev.ma
Mons. Damian ZIMON
Arcivescovo Metropolita di Katowice
ul. Jordana 39
40-953 KATOWICE

Sura ya nne



CONGREGAZIONE
DELLE CAUSE DEI SANTI

R7p. I. 191unil A.D. 19S

Prot. N. 2232-1/98

Excellentissime Domine,

Literis, die 22 mensis Aprilis huius anni 1998 editis, Excellentia Tua ab h
Congregatione de Causis Sanctorum quaeris utrum ex parte Sanctae Sedis aliqu
obis causae Beatificationis et Canonizationis Servae Dei MARIA
DULCISSIMAE (in saeculo: Helenae Ioanae Hoffmann), Sororis profess
Congregationis Sororum i Maria Immaculata, quae vita anno Domini 1936 fuit
est.

Re explorata, placet mihi Excellentiam tuam certiore reddere ex pal
Sanctae Sedis NIHIL OBSTARE quominus Causa Beatificationis et Canonizationis
eiusdem Servae Dei Mariae Dulcissimae (in saeculo: Helenae Ioanae Hoffmann)
peragi possit, servatis "Normis servandis in Inquisitionibus ab Episcopis racion
in Causis Sanctorum". die 7 mensis Februarii anno 1983 ab eadem Congregatio
editis.

Excellentiae tuae addictissimus
in Domino

+ Iosephus Saraiva Martins
Archiep. tit. Thuburicensis
Praefectus

+ Eduardus Nowak

+ Eduardus Nowak
Archiep. lit. Lunensis
Secretarius

Exc. loc. : Rev. iiii DOMINICO
o. 110 DAMIANO ZIMON
Archiepiscopo Katowiceusi
ul. Jorkillilil. 39
40-043 Katowice
Tel. -11 A

Baraza la Kitaifa la Maaskofu lililokutana huko
Warsaw mnamo Marchi 1998, lilikubali kuanza kwa

Sura ya nne

mchakato huo. Hati muhimu zilipelekwa Roma vile vile. Mwezi Juni mwaka ule ule majibu bayana yalirudi. Mchakato wa kumtangaza Sista Dulcissima uliweza kuanza tarehe 18 Februari 1999 kwenye chumba cha chini ya ardhi cha Kanisa Kuu la Kiaskofu la Katowice. Maadhimisho yaliongozwa na Askofu Mkuu Damian Zimon wa Mji Mkuu wa Katowice. Kabla ya Misa, kikao cha kwanza cha mchakato kilifanyika. Watu ambao wangeongoza hamasa waliapishwa. Mdaawa wa usababisho alikuwa Padre Alojzy Drozd.

Kwenye maadhimisho walishiriki Askofu Gerard Bernecki na Askofu Stefan Cichy – Maaskofu wa Katowice, pamoja na idadi kubwa ya Masista wa Shirika la Maria Immakulata. Ndugu wa Sista Dulcissima pamoja na watu wengi sana toka Brzeznie na Zgoda pia walikuwepo. Matangazo ya Idara ya Kitume na ya Mji Mkuu wa Katowice yalisomwa mbele yao.

Sura ya nne

HITIMISHO

Lengo la kazi hii ni kuelezea maisha ya Mtumishi wa Mungu Sista Dulcissima Helena Hoffmann na jitihada zake za kuuendea utakatifu. Ndiyo maana kwa hakika mlolongo mzima wa matukio yanayohusiana na mada hii hauchoshi. Sherehe ambayo tumeisherehekea miongoni mwa mambo mengine ya awali ni kuufukua mwili wa Sista Dulcissima na kuanza mchakato wa kumtangaza Mwenyeheri. Hii si tu nafasi ya kusherehekea au kujikusanya, bali ni kuonesha hitaji la kujua kwa karibu kuhusu mtawa huyu mtakatifu. Uhaba wa taarifa kwenye tarihi ni sababu iliyopelekea baadhi ya sura za kazi hii kuwa za juu juu tu.

Kwenye baadhi ya sura maalum za kazi hii vipengele vifuatavyo vimeelezwa: kipindi cha maisha ya utoto wa Mtumishi wa Mungu, mawasiliano yake ya karibu na Masista wa Maria, kupokelewa kwake Shirikani na malezi ya maisha ya kitawa ambayo yalifanyika katika upostulanti na unovisi, ambapo baadaye aliweka nadhiri zake za kwanza na kisha nadhiri za daima. Kipindi hicho kwa Sista Dulcissima ulikuwa ni muda wa sadaka na mateso ambayo aliyapokea kwa upendo wa Yesu. Pili, umeelezwa mvuto wa Mtakatifu Theresa wa Lisieux ambaye Sista Dulcissima alikuwa akiongea naye; mvuto wa maisha ya kiroho ya Sista Dulcissima na uhusiano wake na watu. Licha ya mateso aliyoyaonja na kifo alichokuwa akikisubiri, aliendelea kuwahudumia watu wengine. Mwisho, ni ibada kwa Sista Dulcissima ambayo inaendelea hadi leo.

Mwandishi anajaribu kutumia ushuhuda na shukrani zilizomilikiwa na Shirika pamoja na dodoso toka kwa watu binafsi waliomfahamu mtumishi wa Mungu au kwa watu waliopata fadhili mbalimbali kutokana na maombezi yake.

Sura ya nne

Tushukuru kwamba hadi sasa ibada kwake zinaendelea na mchakato wa kumtangaza Mwenyeheri umekwishaanza kama ulivyoelezwa kwenye sura ya mwisho.

Kwa nini Sista Dulcissima anakuwa ni mada ya kitabu hii?

Zipo sababu mbalimbali: Kwanza, Nimetumia muda wa miaka mitatu kama sista huko Brzezic, nikiishi na kufanya kazi kwenye nyumba ambayo Sista Dulcissima aliishi na kufia. Wakati huo niliweza kuona na kutazama ibada ikienea. Nyakati za jioni sana niliona mara nyingi kupitia dirishani kwamba kulikuwa na mtu akisali kwenye kaburi la Sista Dulcissima na mishumaa ilikuwa ikiwaka muda wote. Na daima kulikuwa na maua mengi mabichi juu ya kaburi lake. Sikumjua sista huyu jinsi alivyokuwa. Nilikuwa nimeambiwa kuhusu yeye na Sista Helena Pokorska ambaye alikuwa akiishi kwenye nyumba yetu wakati ule. Alinieleza ni nini kilikuwa kinatokea baada ya kifo cha Mtumishi wa Mungu na vile vile heshima aliyopewa na watu. Kuona hayo yote sikujua kuwa mimi pia nilianza kushiriki kwenye ibada hii. Mimi mara nyingi, karibu kila siku, nilikwenda maziarani ili nisali mbele ya kaburi lake.

Sababu ya pili ni kufukuliwa kwake ambako kulifanyika 8/4/2000 kwenye makaburi huko Brzezic. Masalia ya udongo ya Sista wetu yalipelekwa kwa maandamano ya ibada toka maziarani mpaka kwenye nyumba ya utawa huko Brzezic. Pale masalia hayo yalithibitishwa na madaktari kwa kiapo, kisha yalihifadhiwa. Halafu jeneza liliwekwa kwenye ushoroba

Sura ya nne

wa nyumba ya kitawa ili watu waweze kuaga. Baada ya hapo, jeneza lilifungwa na kuzibwa. Mazishi ya pili yalifanyika sio kwenye ile sehemu ya zamani bali kwenye sehemu ya kaburi lililotayarishwa kwenye kanisa la parokia huko Brzezie. Maadhimisho yaliongozwa na Askofu Mkuu Damian Zimon. Baada ya kulitabaruku kaburi sanduku liliwekwa mle ndani na kuzibwa kwa matofali. Kisha watu wote walioshiriki mazishi walikwenda kanisani kwa ajili ya Misa iliyoshirikisha mapadre waliokuwepo chini ya uongozi wa Jimbo Kuu la Katowice, wakiomba kwa ajili ya kutangazwe kuwa Mwenyeheri, Mtumishi wa Mungu Sista Dulcissima Helena Hoffmann.

Sababu ya tatu ni ukweli kwamba, mimi pamoja na Sista Dulcissima tulijiunga na Shirika moja la Masista wa Maria Immakulata.

Sura ya nne



Picha ya kibali cha kusafiria

**Kanisa la Parokia
la Zgoda**




**Chumba
cha Sista
Dulcissima
huko
Brzezie**



Sura ya nne

**Msalaba na medali ya Sista
Dulcissim**



Kanisa sasa ya Masista huko Brzezic

Sura ya nne

Nyumba ya Masista huko Nysa



Kanisa huko Nysa

Sura ya nne

Kaburi nyuma ya nyumba ya Masista wa Maria Immakulata huko Brzezie



Kaburi la Sista Dulcissima leo



Sura ya nne





Sura ya nne

Familia ya Sista Dulcissima



Parokia huko Brzezie

Sura ya nne

Mimi tarehe 25 Novemba mwaka 2010 kwenye kaburi ya Sista Dulcissima



Sura ya nne

MAJADILIANO YA MTUNZI NA WATU **MBALIMBALI**

Ushahidi wa Bibi Goralczyk.

Mwezi wa pili mume wangu aliumwa pingiri ya kuiuno. Mwezi Machi ikaongezeka varix. Zaidi ya hayo aliumwa pumu, mpaka kutema damu. Mganga alisema kuwa kifo kinakaribia na saa yoyote anaweza kufa. Mgonjwa akapelekwa hospitali na baada ya uchunguzi Daktari Beker alisema kwamba mgonjwa mwenye umri wa miaka hamsini na shida kama hii kwa uwezo kibinadamu hawezi kupona, lakini Mungu yupo. Mimi ikiwa mke wake lazima kujiweka tayari kwamba kifo kimekaribia. Baada ya kuchukuliwa picha ya mionzi ilionekana kuwa moyo ulizidi kupanuka. Kilichobaki ni kumomba Mungu, ndivyo nilivyofanya na watoto wangu. Hata hivio shida imezidi siku hata siku. Katika mahangaiko nilianza kumwomba Sista Dulcissima kuwa na matumaini kwamba asikilize maombi yetu, na bwana wangu, baba ya watoto watatu apone. Tarehe 17 mwezi wa Machi katika nyumba ya utawa huko Brzezic padre alisali Misa Takatifu kwa kumomba Sista Dulcissima amsaidie kwa maombezi yake mgonjwa apate afya njema. Siku ya pili tarehe 18 mwezi huu wa tatu aliacha kutapika damu na kila siku ilionekana nafuu. Hatari ya kifo imepita. Tarehe 10 mwezi wa Julai alipata ruhusa kurudi nyumbani yu mzima.

Ushahidi wa Bibi Lusja Bugdol

Nilimjua Sista Dulcissima alipofika muda ule huko Brzezic. Wakati ule mimi nilikuwa na umri wa miaka nane. Mama yangu mzazi alifahamiana na Masista Utawani na

Sura ya nne

aliwasaidia kazi ndogondogo. Zaidi alipanga urafiki na Sista Lazaria ambaye alimuguza Sista Dulcissima wakati wa ugonjwa wake. Mara nyingi Masista wote wawili walifika nyumbani kwetu hasa muda walioumwa kaka zangu kwa ugonjwa wa tatizo la kupumua. Yohane kaka yangu mmoja kati ya hao wawili alizidiwa sana, alianza kuwa kipofu, bubu na aliumwa uti wa mgongo. Daktari alitueleza kwamba hakuna matumaini yoyote ya kupona. Sista Dulcissima alifika kila siku kumwona mgonjwa na kumuomba Mungu, alisali: “Mungu Mwenyezi nakuomba uchukue jicho langu moja na ukampatie kijana huyu aone.” Ulifanyika muujiza, kaka yangu ameanza kuona, kusikia na pole pole alipata afya njema. Sisi hatukujua mambo haya isipokuwa baada ya kifo cha Sista Dulcissima, Sista Lazaria kafunuliwa siri hii kuwa kaka yetu amepata nafuu kwa maombezi ya Sista Dulcissima. Sista alisali na amepata ufunuo kama kijana hatakuwa kichaa, kipofu wala bubu. Lakini kwa nguvu za sala zake Sista Dulcissima amepata salama na kuepuka na msalaba mkubwa wa maisha yake. Kaka yangu anafahamu shauri hili na anayo shukrani kwa hayo yote yaliyomtokea.

Mimi ninamkumbuka Sista Dulcissima katika ugonjwa wake ambaye mwenyewe alishindwa kutembea lakini kwa msaada wa Sista Lazaria na fimbo lake alijikokota kuja kuwaona kaka zangu wagonjwa. Hayo yote alifanya katika mapendo na kila neno lililotoka moyoni mwake lilileta matumaini na imani. Sala zake siku zote zimefanikiwa na kuleta matunda ya manufaa. Sista Dulcissima alipokufa nilikuwa na umri wa miaka kumi na moja. Mazishi yake yalikuwa na maandamano makubwa sana na mimi mwenyewe nilibeba taji za maua mbele ya jeneza. Paroko katika parokia yetu Padre Feliks Borzucki alisali Misa ya mazishi. Alivaa mavazi meupe, katika mahubiri yake alitamka kwamba: “Alikufa Mtakatifu kwa

Sura ya nne

hiyo haifai kusikitika” Wakati maandamano kuelekea makaburini badala ya kuimba nyimbo za masikitiko watu waliimba utenzi Magnificat.

Sista Dulcissima wakati yuko hai aliombea Parokia yetu na mpka leo anatuombea mbele ya Mungu. Watu wengi walipata neema nyingi na kupona kabisa kwa maombezi yake. Kwenye kaburi lake yalipandwa maua ya waridi, na maua haya hutoa harufu mzuri. Watu wengi kwa imani yao walichuma majani ya waridi kwa imani kuwa yanasaidia kwa shida mbali mbali. Wengine huchota udongo kwa imani una nguvu ya kukinga hatari za maisha. Wengine kuweka udongo ndani ya gari na kuomba Sista Dulcissima awasaidie wakati wa safari zao. Mwanangu – anashuhudia bibi Lusia – wakati wa kurudi kutoka likizo Italia amepata ajali. Gari mbili ziligongana kiasi cha kuharibika kabisa, lakini watu wote walitoka salama na kuamini kwamba udongo kutoka kaburi ya Sista Dulcissima ulikuwa ndani ya gari mesalimisha watu. Imani ya nguvu ya udongo huu wa kaburini imeenea pote hata wakati wa vita ya pili 1945 sio raia tu bali hata maaskari walichota ili wapate kurudi nyumbani salama kutoka vitani.

Ninakumbuka pia simlizi moja iliyotokea katika familia yetu. Mwaka 1936 mwezi wa tatu alizaliwa dada yangu mdogo aliyeitwa Teresia. Siku ya Ubatizo Sista Dulcissima alimletea zawadi ya medali yake na akasema kwamba atakuja kumchukua mbinguni wakati wake. Sista Dulcissima alikufa mwezi wa Mei 1936 na mwaka uleule mwezi wa Octoba alikufa mdogo wangu. Iliaminika kuwa kweli Sista Dulcissima alikuja kumchukua kama alivyosema. Medali hii mpaka leo inatunzwa katika familia yetu kwa heshima kubwa. Kila mara jirani wanakuja kuchukua medeli hii na kuwavesha wagonjwa na wengi kwa nguvu zake wanapona kabisa.

Sura ya nne

Barua ya Bwana Yohana Darowski anayekaa London.

Wakati wa baridi huko Ulaya siku moja nilicheza na ndugu yangu muda mrefu nje. Ubaridi ulitubana sana mpaka tulipata homa kali sana. Tulianza kuumwa sana hasa mimi nilizidiwa sana. Nilipata uti wa mgongo. Nilikuwa kipofu na bubu muda mrefu sana na sikujua kitu kilichofanyika nje ya utashi wangu. Niliona giza tu na nilijisikia kama mtu ametumbukizwa kwenye shimo kubwa sana. Nilibaki na fahamu ya kunusa na kupapasa. Pia niliweza kuongea. Kwa maombezi ya Sista Dulcissima ulifanyika muujiza. Mimi nilianza kuona na yeye alikuwa kipofu. Daktari alipoona haya alimwambia mama yangu kwamba yemefanyika mambo makubwa yasiotafsiriwa kwa nguvu za kidunia.

London, 25.02.1996

Ushahidi wa Beata Wicisk.

Mwaka 1945 mara baada ya vita ya pili niliwatembelea wagonjwa. Siku moja nilimkuta mama fulani Maria mwenyeji wa kijiji cha Brzeznie alikuwa mgonjwa sana. Bwana wake alikuwa bado hajarudi kutoka vitani na yeye alibaki na watoto wadogo wanne bila msaada. Dada yake alipoona hali ya mdogo wake ni ngumu na mwenewe ni mzee na afya hafifu akapata mawazo kwamba atakapofariki mdogo wake, mwenyewe atashindwa kuwalea watoto wake. Alienda kaburini kwa Sista Dulcissima na alimwomba akamchukue badala ya mdogo wake lakini aliomba kwanza apate bahati ya kumuona mwanae akirudi kutoka vitani. Kweli mambo yalifanyika. Mtoto wake akarudi, yeye mwenyewe aliumwa na kufa kama alivyoomba na mdogo wake akapona na kuwalea watoto wake. Hata bwana wake

Sura ya nne

alirudi pia kutoka vitani. Muda huu yalipofanyika mambo haya nilikuwa na umri wa miaka 16. Pia nilishuhudia mazishi ya Sista Dulcissima na watu wengi mara baada ya kifo chake walimheshimu kama Mtakatifu.

Alipoumwa mama yetu mzazi tulimjia Sista Lazaria ili atusaidie kusali na kuomba kwa maombezi wa Sista Dulcissima ili mama yetu apone. Wakati wa kusali Sista Lazaria alisikia sauti moyoni mwake kwamba mama yetu hatapona, kwa sababu Mungu anamtaka kwake. Aliacha watoto tisa yatima lakini imani yetu imeimarishwa zaidi na tulipokea uamuzi wa Mwenyezi Mungu.

Nilipokuwa na umri wa miaka 49 nilifanya kazi chekechea. Siku moja katika mguu wangu ilipasuka mshipa na madaktari walinikatisha tamaa kupona. Lakini mimi mwenyewe sikukata tamaa bali nilimwomba mama moja aniletee jani moja kati ya maua yaliyoota kaburini kwa Sista Dulcissima. Lilipoletwa jani chumbani kwangu ikaenea harufu nzuri sana ya kupendeza na mguu wangu ulipona saa ile ile. Wote walipoona mambo haya walistaajabu sana na waligundua kuwa huu ni mwujiza. Nilipotimiza miaka 58 niliumwa sana na kutoka damu. Ukapita uamuzi niende kwenye opereshini. Niliogopa sana. Nilikwenda kuzuru kaburi la Sista Dulcissima kuomba msaada. Wakati wa sala nilisikia sauti: hutapata operesheni. Kweli nilianza kupona kidogo kidogo na kupata usalama kabisa kwa njia ya maombezi ya Sista Dulcissima. Katika familia yangu siyo mimi peke yangu napata msaada wake bali hata kaka zangu na wengineo.

Ushahidi wa Theresa Czajka

Nilikuwa na umri mdogo sana wakati alipoishi Sista Dulcissima duniani, lakini ninamkumbuka sana. Mara

Sura ya nne

nyingi nilimtembelea. Wakati huuo Sista alikuwa anaumwa, lakini bado alifanya kazi ndogo ndogo, kama kushona nguo za watoto na kufuma. Nilimpenda sana Sista Dulcissima. Baada ya kifo cha Babu yangu nilifikiri masista walisababisha Babu yangu aondoke kwa hiyo niliwachukia masista. Wakati wa mazishi ya Sista Dulcisima nilikuwa kwenye maandamano na kubeba mapambo.

Ushahidi wa Kazmir Darowski

Nilipotimiza umri wa miaka 18 wanajeshi wa Urusi walitaka kuniteka na kupeleka Kazakstni kwenye kambi ya wakimbizi, lakini niliokoka. Nilikuwa kwa shangazi yangu huko Ploni .Walipofika Maaskari Warusi nilijificha chini ya kitanda chumbani kwa shangazi yangu. Walipoingia ndani ya chumba kwa nia ya kunikamata walinitafuta kwenye kabati kikubwa. Walitoa nguo kutoka kabatini, wakondoa mashuka kutoka kitanda kile na kuvuruga chumba, lakini chini ya kitanda hawakuangalia. Kwa hiyo, ninaamini Sista Dulcissima aliniokoa.

Ushahidi wa Bibi Maria Pokracka

Alipokufa Sista Dulcisima nilikuwa na umri wa miaka 11. Nakumbuka vizuri mazishi yake.

Baada ya miaka mingi kupita, nilipokuwa mtu mzima na kufunga ndoa nilipata mimba. Kama kawaida nilifanya kazi nzito kwa kulima shamba langu. Siku moja baada ya kazi nilienda kanisani kwenye ibada. Nilipokuwa kanisani nimepata maumivu makali. Watu walinipeleka hospitalini. Daktari aliamua haraka kufanya upasuaji. Nilipolazwa kwenye meza ya operesheni nililia kwa sauti kubwa na kusema:” Sista Dulcissima ushike kisu kile” Maneno hayo

Sura ya nne

alisikia Sista mmoja aliyekuwa akimsaidia daktari wakati wa opereshieni. Saa tatu daktari alifanya kazi ya upasuaji. Kesho yake alifika yule Sista aliyekuwa akimsaidia daktari. Aliniuliza juu ya maneno niliyosema kabla ya kupata operesheni. Nilimweleza juu ya Sista Dulcissima na kusema: sisi wanakijiji cha Brzeze tunamuamini sana na kumwomba Sista Dulcissima atusaidie. Na kila tunapomwomba msaada wake tunapata neema. Nami nilimwomba ashike kisu ili daktari afanye upasuaji vizuri na kwa ajili ya afya yangu. Yule Sista alistaajabu na kusema “kweli muujiza ulitendeka.’ Pia daktari alikiri kwamba hali yangu ilikuwa ngumu sana. Naye naamini ni muujiza.

Ushahidi wa Bibi Kunegunda Grycman

Nilipokuwa mtoto wa umri miaka 8 nilimtembelea Sista Dulcissima. Alinipatia doli kubwa ili nichezee. Yeye wakati huo alikuwa mgonjwa, lakini bado alitembea pole pole na kuwatembelea wajonjwa wengine na majirani. Ninakumbuka vizuri siku ya mazishi ya Sista Dulcissima.

Nilipokuwa na umri wa miaka 17 tulitekwa kutoka Brzezie na wanajesh wa Urusi na kuchukuliwa kwa kupelekwa Sibir. Kwanza walitupeleka mjini Rybnik. Kutoka huko kwa miguu tulienda mpaka Branice kwenye kambi ya wakimbizi. Njiani tulisali na kuomba Mungu. Niliambatana na Bibi mmoja na kusali. Tulipokuwa kwenye kambi tuliambia na yule Bibi ili tutoroke. Tulifanikiwa kidogo sana sababu tulikamatwa njiani na wanajesh wa Urusi, lakini wawo walikuwa wema. Walitusaidia kupata nyumba na kupumzika. Usiku uleule tuliingiliwa na wanajesh na kuhojiwa. Mara nyingi walifika usiku na kutuhoji na kuuliza maswali. Wakati huu mgumu nilisali sana kwa maombezi ya Sista Dulcissima ili tupate salama na

Sura ya nne

uhuru. Maombi yetu yalisikilizwa na Mungu. Tulipata uhuru na kurudi nyumbani salama.

Ushahidi wa muuguzi moja katika hospitali

Sista Dulcissima alisikiliza sala zetu kwa hiyo ninapenda kutoa shukrani. Pia natoa ushuhuda jinsi alivyo alimwoko mgonjwa moja katika hospitali yetu huko Katowice. Mgonjwa huyo alilazwa katika hospitali yetu tangu 24/1/1997. Miaka arobaini alimuasi Mungu, hakuwapokea sakramenti. Zamani alijiunga na chama cha ZMP – chama cha vijana ya ukomunisti. Baadaye alikuwa mojawapo wa chama cha tawala PZPR- chama cha wakomunisti. Chama hicho kiliopinga dini na kutawala kwa mabavu.

Alipoumwa na kulazwa hospitalini mke wake pamoja nasi tulimshawishi ageuze mwenedo wake na amshuhudie Mungu, kwani tuliona dalili ya kuelekea kwenye neema na utu. Lakini wapi? Tulishindwa wote. Kila siku padre Benedikto Zowada aliwatembelea wgonjwa, pia Paroko Janusz Kwapiszewaki alikuja kuwaletea wgonjwa Sakramenti ya Ekaristi. Mapadre hao pia waliongea na mgonjwa wetu bila mafaniko. Mama yangu na mimi tuliamua kusali na kumwoba Sista Dulcissima atusaidie kumwombea mgonjwa huyo Yohane. Usiku tarehe 7 kuamkia tarehe 8 mwezi wa pili hali yake mgonjwa ilikuwa mbaya. Nguvu yake ilipunguwa sana hata hajaweza kuongea vizuri. Kuanzia tarehe 21 hajaweza kumeza hata dawa. Alikuwa na maumivu makali. Katika hali hii mbaya bado alikataa kuungama na kupokea sakramenti. Padre Benedikto mara kwa mara alimtembelea, lakini yeye daima alikataa. Sisi tulisali na matumaini yetu tuliweka kwenye maombezi ya Sista Dulcissima. Ni kweli, sala zake na maombezi yake

Sura ya nne

kwa Mungu zilileta uongofu. Yule mjonjwa tarehe 27 mwezi wa pili aliungama na kupokea sakramenti ya Ekaristi na mpako ya wagonjwa. Mke wake, kaka yake, shemeji yake na mimi tulishuhudia neema aliyompata mgonjwa wetu. Jioni tulipokuwa yeye na mimi tu nilimuuliza.” Je, unafurahi? Pia nilitaka kupata uhakika wa tukio hilo na nilimuuliza.” Je, ulipokea sakramenti kwa hiari yako, au sisi tumekulazimisha?” Mgonjwa alitamka kwa nguvu na vizuri sana “Ndiyo nilipokea kwa hiari yangu” Siku zilizofuata alipokea sakramenti ya Ekaristi. Alifariki 5/3/1997 kwa utulivu sana ingawa alikuwa na maumivu makali.

Watu wengi wangependa kutoa ushuhuda juu ya neema nyingi walizozipata. Sista Dulcissima wakati wa maisha yake hapa duniani alipata mateso mengi. Mateso haya aliyapokea kwa ushujaa na utulivu. Katika mateso yake alijitoa kwa Mungu bila kujibakiza ili kuwasaidia watu na kuziokoa roho zao. Watu alimwona Sista Dulcissima Mtu Mkubwa, sababu kwa sala zake wao wamepata neema na miujiza. Kumbe Sista huyo ni Mtawa kama Watawa Wengine. Wajibu wa kila Mtawa ni kuwaombea watu wote na kuwa waaminifu kwa wito walioupata.

Wengi wao waliotoa ushahidi walimfahamu Sista Dulcissima wakati alipoishi hapo duniani. Wengine waliosikiliza ushuhuda wa wenzi wao na kusali hatimaye walipata neema. Kumbukumbu zote za ushahidi uliotolewa na watu kwa mwandishi zinatunzwa na Shirika hili huko Katowice. Tujiunge na juhudi ya kumwomba Mwenyezi Mungu ili Sista Dulcissima atangazwe Mwenye Heri .

Sura ya nne

Sura ya nne

SALA KWA AJILI YA KUOMBA, MTUMISHI WA MUNGU SISTA M. DULCISSIMA ATANGAZWE MWENYE HERI

Mungu, Baba Mwenye huruma nyingi, umewapatanisha wanadamu wote pamoja nawe, kwa kifo na ufufuko wake mwanao wa pekee, Yesu Kristo. Uwaalike waamini wote wayaunganishe mateso yao pamoja na mateso yale ya mwokozi Yesu, kwa manufaa ya Kanisa, mwili wake wa fumbo. Upokee kama sadaka inayokubalika, maisha yaliyomjaa unyenyekevu mtumishi wako Sista Maria Dulcissima aliyebeba kwa furaha msalaba wake kila siku. Umvike taji la utukufu wao wenye heri katika utawala wako, na pia uyapokee maombi yao wana-taifa lako wanaoleta kwako kupitia maombezi yake. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amina.

MAANA ZA VIFUPISHO

- ACGSM Archiwum Domu Generalnego Siostr Maryi (Ofisi ya Nyaraka za Kumbukumbu za Nyumba Kuu ya Masista wa Maria)
- ADMSMNW Archiwum Domu Macierzystego Siostr Maryi Niepokalanej we Wroclawiu (Ofisi ya Kumbukumbu za Nyaraka za Nyumba ya Masista wa Maria Imakaulata huko Wroclaw)
- APSMNK Archiwum Prowincjonalne Siostr Maryi Niepokalanej w Katowicach (Ofisi ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Provinsi ya Masista wa Maria Immakulata huko Katowice)
- ASMNW Archiwum Siostr Maryi Niepokalanej we Wroclawiu (Ofisi ya Kumbukumbu za Nyaraka za Masista wa Maria Immakulata huko Wroclaw)
- KDK Konstytucja Dogmatyczna o Kosciele (Mafundisho Sadikifu ya Kanisa)
- ZPA Zbioty prywatne autorki (Makusanyo Binafsi ya Mtunzi)

VITABU VYA REJEA

Rejea za Kumbukumbu za Nyaraka

1. Archiwum Domu Generalnego Siostr Maryi (Ofisi ya Kumbukumbu za Nyaraka za Nyumba Kuu ya Masista wa Maria,
 - Prot. N. 109/95:
 - Kumbukumbu za Sista Dulcissima, Prot. N. 104/95
2. Archiwum Domu Macierzystego Siostr Maryi Niepokalanej we Wroclawiu (Kumbukumbu ya Nyaraka za Nyumba Mama ya Masista wa Maria Immakulata huko Wroclaw)
 - Tangazo la Jarida la Mama Mkuu, Toleo la I, 1969.
 - Matukio ya Kila Siku ya Shirila la Masista wa Maria Immakulata, 1854-1909.
3. Archiwum Prowincjonalne Siostr Maryi Niepolanej w Katowicach (Ofisi ya Kumbukumbu za Nyaraka za Provinsi ya Masista wa Maria Immakulata huko Katowice)
 - Matukio ya Kila ya Siku ya Provinsi ya Poland ya Shirika la Masista wa Maria Immakulata, 49-50
 - Mashuhuda wa Masista wa Maria Immakulata kuhusu Sista Dulcissima
 - Kutoka Parokia ya Mtakatifu Yosefu huko Zgoda 1890-1927, Kitabu cha Ubatizo 1910, namba 110
4. Archiwum Siostr Maryi Niepokalanej we Wroclawie (Ofisi ya Kumbukumbu za Nyaraka za Masista wa Maria Immakulata huko Wroclaw), Toleo la III, 1930-1950

Sura ya nne

Rejea za Machapisho

BALCHAN, A., *Uzdrowiajacy aspect spotkania z Bogiem u narkomanow na podstawie przeprowadzonych badan*, Lublin-Katowice 1988, maszynopis

Vitabu

BANIK, E., *W sluzbie Niepokalanej* Krakow 1994

Magazeti

DOMINIKA, J., "Swieta z Brzezie Cudowna ziemia", *Gazeta Wyborcza*, IV 1999

Majadiliano ya Mtunzi na Watu Mbalimbali

Na Bi. Lusja Budgol tarehe 04 Mei 1999

Na Bi. Teresa Czajka tarehe 04 Mei 1999

Na Bw. John Darowskim tarehe 04 Mei 1999

Na Bw. Kazmir Darowskim tarehe 04 Mei 1999

Na Bi. Kunegunda Grycman tarehe 04 Mei 1999

Na Bi. Maria Pokracka tarehe 04 Mei 1999

Na Bi. Beata Wycisk tarehe 04 Mei 1999